# Nipashe

Jumamosi Juni 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581715

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



**Daktari** adaiwa kughushi nyaraka bima ya maisha ya marehemu rafiki yake

UKURASA 3



**Fisi** aua mtoto mgongoni mwa mama

UKURASA 7



**Putin** aonya Korea itajuta ikiipa silaha Ukraine

UKURASA 17



UKURASA 11

ALIISHI JICHO MOJA HALIONI

MAUAJI WENYE UALBINO

# Maaskofu: Kiini chake hiki hapa



"Ni kweli padri huyo ni wa Jimbo Katoliki Bukoba na tumemsimamisha kutoa huduma zote za kichungaji mpaka..."

ASKOFU JOVITUS MWIJAGE

UKURASA 2

"Watu wawe wanyenyekevu na wenye hofu mbele ya Mungu ili kuwa na jamii bora."



ASKOFU ALEX MALASUSA

"Mauaji ya wenye ualbino, vitendo vya ushoga na ulawiti vinaanzia kwenye familia."



DK. FANUEL SHEKIHIYO

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### UTAFITI: UTITIRI HUU WA TOZO NI HATARI



SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI) limesema kuwapo utitiri wa tozo katika kila mkoa na halmashauri kumekuwa kikwazo katika ustawi wa biashara na uwekezaji nchini...

## Mke adaiwa kummwagia maji ya moto mumewe

UKURASA 15




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiongoza waombolezaji kuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Tixon Nzunda, nyumbani kwake Goba, Dar es Salaam, jana. **Habari zaidi Uk. 5. PICHA: OWM**

# Sukari moto bungeni

- **Wabunge** wataka sheria ifumuliwe kubana vigogo ... *Uk. 5*


**MICHEZO** SIMBA SC, COASTAL ZAMGOMBEA LAWI UK.24

**MAONI,** UK.6



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipima afya, wakati wa zoezi la upimaji afya bure, lililofanyika katika viwanja vya Kigogo Barafu, jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kiini mauaji wenye ualbino hiki hapa

**Faustine Feliciane na Jeniffer Gilla**

MWANGALIZI Mkuu mpya wa Kanisa la Pentekoste Tanzania, Dk. Fanuel Shekihiyo, ameshauri viongozi wa dini wenzake na jamii kujikita katika utatuzi wa matatizo ya kifamilia, akiamini hayo ndiyo kiini cha vitendo vya ukatili vinavyoshika kasi nchini hivi sasa, yakiwamo mauaji ya watu wenye ualbino.

Kukitolewa rai hiyo, Kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba limetangaza kumsimamisha Padri Elipidius Rwegoshora kutoa huduma za kichungaji kutokana na kukabiliwa na tuhuma za kuhusika katika mauaji ya mtoto mwenye ualbino, Asimwe Novart aliyekuwa na umri wa miaka miwili na nusu.

Katika ibada maalum ya kumuaga mtangulizi wake, Dk. Philemon Tibanenason kwenye Kanisa la Pentekoste Kiluvya, Dar es Salaam jana, Dk. Shekihiyo alisema jamii ikimtegemea Mungu haiwezi kuingia katika uovu kama uliofanywa dhidi ya mtoto mdogo asiye na hatia.

Dk. Shekihiyo alisema matatizo yote yanayotokea, yakiwamo ya mauaji ya watu wenye ualbino, ushoga na ulawiti, yanaanzia katika familia, hivyo ni lazima matatizo hayo yashughulikiwe na jamii na watumishi wa Mungu bila kujali dini.

"Haya mauaji ya binadamu wenzetu wenye ualbino, kwa asilimia kubwa yanatokana na ushirikina. Haya yote yanaanzia katika familia zetu. Kwa watumishi wa Mungu, tunapaswa kuongeza maombi kuziombea familia na jamii kuachana na matendo haya ya kishetani," alisema Dk. Shekihiyo.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema alimpongeza mtangulizi wake, Dk. Tibanenason kwa utumishi wake wa miaka 58 ndani ya kanisa hilo.

"Umejenga kanisa imara, umeonesha namna gani kiongozi wa dini anapaswa kuwa, maisha yako ya uongozi ni funzo kubwa kwetu sisi ambao tunaendeleza pale ulipoachia, bado kanisa litahitaji ushauri wako siku zote," Dk. Shekihiyo alisema.

ASKOFU MALASUSA

Katika ibada hiyo, Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa alisema kuna haja watu kuwa wanyenyekevu na wenye hofu mbele ya Mungu ili kuwa na jamii bora.

Askofu Dk. Malasusa ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, alisema Dk. Tibanenason ambaye amestaafu akiwa na umri wa miaka 81, alikuwa kiongozi mwenye unyeyekevu na aliyeunganisha madhehebu mbalimbali katika umoja wao wa Mkoa wa Dar es Salaam.

"Tunashukuru kwa maono yake ya kulileta kanisa pamoja bila kujali madhehebu, kwetu amekuwa mwalimu wa kweli na ingependeza kama Pentekoste mtaandaa kitabu chake," Askofu Dk. Malasusa alishauri.

Akizungumza wakati akitoa hotuba yake ya kuaga, Dk. Tibanenason alisema siku zote alikuwa akiomba amalize kazi ya Mungu katika heshima yake.

"Ninaondoka huku kanisa tayari likiwa na viongozi wake walioanza kazi, hivi sasa na mimi nipo tayari kuongozwa," Dk. Tibanenason alisema.

**PADRI ASIMAMISHWA**

Taarifa iliyotolewa jana na gazeti Kiongozi linalomilikiwa na Kanisa Katoliki, ilieleza kuwa Askofu wa Jimbo Katoliki Bukoba, Jovitus Mwijage, ametangaza uamuzi wa kumsimamisha kazi padri huyo mpaka pale suala lake litakaposhughulikiwa kisheria.

Katika taarifa hiyo, Askofu Mwijage alinukuliwa akisema ni kweli padri huyo ni wa Jimbo la Katoliki Bukoba, hivyo wamesikitishwa kusikia kuwa ni miongoni mwa watuhumiwa wa mauaji ya mtoto mwenye ualbino.

"Ni kweli padri huyo ni wa Jimbo Katoliki Bukoba na tumechukua uamuzi wa kumsimamisha kutoa huduma zote za kichugaji mpaka hapo suala lake litakaposhughulikiwa na vyombo vya sheria.

"Baada ya vyombo vya sheria kumaliza kazi yake, ndipo taratibu nyingine za kanisa zitafuata," Askofu Mwijage alinukuliwa na gazeti hilo.

Asimwe, mtoto mwenye umri wa miaka miwili na nusu, alinyakuliwa mikononi mwa mama yake na watu wasiojulikana Mei 30 mwaka huu katika Kijiji cha Bulamula, wilayani Muleba, mkoani Kagera na baadaye kupatikana katika karavati wilayani Muleba ukiwa hauna baadhi ya viungo.

Watu tisa, akiwamo Paroko Msaidizi wa Bugandika, Elipidius Rwegoshora, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi wakituhumiwa kuhusika na mauaji ya mtoto huyo huku wakidaiwa kukutwa wamevihifadhi viungo vinavyodhaniwa vya mtoto huyo katika vifungashio vya plastiki. Inadaiwa na Jeshi la Polisi kuwa watuhumiwa hao walikuwa wanatafuta mteja.

Mbali na paroko msaidizi huyo, watuhumiwa wengine ni pamoja na Elipidius Rwegoshora, mganga wa jadi; Desideli Evalist, mkazi wa Nyakahama; na Novart Venant, baba mzazi wa mtoto Asimwe.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), polisi wakishakamata mtuhumiwa, wanapaswa ama kumfikisha mahakamani ndani ya saa 24 tangu walipomkamata au kumwachia huru, isipokuwa kwa makosa ambayo yanahusiana na adhabu ya kifo. Tuhuma zinazowakabili, zikithibitika adhabu yake ni kunyongwa hadi kufa.

# Maofisa Habari wa Serikali watoka na maazimio manne

**Na Jenifer Gilla**

KIKAO cha Maofisa Habari wa Serikali kimeazimia mambo manne, ikiwamo kuongeza kasi ya utoaji taarifa kwa wananchi kuhusu utekelezaji miradi ya maendeleo kwa kutumia mbinu za kisasa kama walivyofundishwa.

Akiwasilisha maazimio hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kufunga kikao hicho, Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, alitaja mbinu hizo kuwa ni kufanya uchambuzi wa kina katika taarifa wanazotoa na kuzingatia misingi yote na weledi ya uandishi wa habari.

Alisema maofisa hao pia wameazimia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Idara ya Habari - MAELEZO, ikamilishe ujenzi wa TEHAMA kwa ajili ya kufanya tathmini ya utendaji kwa vitengo vya mawasiliano ya wizara zote na mamlaka ya serikali za mitaa.

Tathmini hiyo pia itahusisha sekretarieti za mikoa, taasisi, wakala na idara zote zinazojitegemea kuanzia mwaka huu wa fedha na pia iangalie mfumo rasmi wa kutoa tuzo katika kikao kazi cha mwaka ujao kwa watakaofanya vizuri.

Maofisa hao pia wameazimia wizara Idara ya Habari - MAELEZO iratibu mafunzo zaidi katika nyakati mbalimbali bila kusubiri mwisho wa mwaka na kongamano, ili kuwajengea uwezo zaidi maofisa hao katika kuleta tija ya kutoa taarifa kwa umma.

Makoba alisema azimio la nne ni kuangalia uwezekana kikao kijacho kifanyike Zanzibar na maandalizi yaanze mapema na kulifanya kongamano hilo kuwa la kimataifa.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye aliahidi serikali itafanyia kazi maazimio hayo huku akiwakumbusha kutumia ujuzi waliopata kuboresha utendaji kazi wao na kuleta mabadiliko katika ofisi zao.

Alisema kazi yao ni kuunganisha serikali, taasisi na umma hivyo majukumu yao makubwa ni kuhakikisha taasisi hizo zinajua yanayoendelea katika jamii, ili kama kuna sehemu wamekosea warekebishe na kuboresha huduma zao.

"Na hapa ni pamoja na kufanya jamii iwe na taarifa sahihi ili ifanye uamuzi sahihi kwa maendeleo yao. Kwahiyo, tuna nguzu zaidi ya hii tunayoizungumza ya kupashana habari, tuboreshe zaidi huduma zetu ili watu wazipende zaidi, waziamini zaidi, tuwajengee imani na huduma tunazotoa," aliagiza

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawaamini na anawategemea kuwa watakwenda kutengeneza taswira nzuri ya serikali, na ndio maana amemwagiza ahakikishe anashughulika changamoto zao.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mohammed Abdulla na Mkurugenzi wa Idara ya Habari - MAELEZO, Makoba wafanye tathmini ya uhitaji wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya maofisa hao na wizara hiyo itahakikisha vinapatikana kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba mwaka huu.

Waziri Nape pia alimwagiza Makoba kujenga utaratibu wa kutembelea taasisi hadi halmashauri zote nchini, kuwasemea maofisa hao na kuhakikisha wanapewa heshima wanayostahili katika maeneo yao kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alimwelekeza afuatilie maslahi ya kundi hilo kwa kuwa wamekuwa wanasumbuliwa katika malipo yao hasa wanapohamishwa vituo vya kazi, hali inayowaharibia maisha yao ya baadaye na kupunguza molari ya kazi.

Waziri Nape pia alimwelekeza kiongozi huyo mpya atengeneze utaratibu wa kuwapatia mafunzo maofisa hao kwenye kanda zao kila mwezi badala ya kutegemea kufanyika mara moja kwa mwaka kupitia kongamano hilo.

## HABARI KITAIFA

# Daktari adaiwa kughushi nyaraka za bima ya maisha ya marehemu

**Na Grace Gurisha**

MFANYAKAZI wa Shirika la Usimamizi wa Maendeleo kwa Afya (MDH), Dk. Martha Tsere, anadaiwa kughushi fomu ya bima ya maisha ya rafiki yake wa karibu, marehemu Tarsila Oisso kwa madai kuwa anatakiwa apewe asilimia 40 ya fedha za bima hiyo ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 400.

Katika shauri hilo la madai namba 11290 la mwaka 2024, mlalamikaji ni MDH na Kampuni ya udalali wa bima ya Busara. Liko Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Shirika hilo limefungua madai dhidi ya Tsere na Justine Edwald ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu ili mahakama iamue nani anastahili kulipwa bima hiyo ya maisha na kwa kiwango gani.

Katika fomu ya warithi ya Group Life Insurance, inadawa Tsere anataka alipwe asilimia 40 ya kiwango cha fedha cha bima hiyo ambayo ni zaidi ya Sh. milioni 400.

Upande wa dalali wa bima hiyo na MDH, unadai kupata wasiwasi inakuaje mtu asiye ndugu kupewa kiwango hicho cha fedha bila ushahidi wowote. Hivyo, ukahitaji uthibitisho zaidi kama kweli marehemu aliandaa fomu hiyo au la.

Katika fomu hiyo ya madai, inadaiwa kuwa uongozi wa MDH uliamua kushirikisha Jeshi la Polisi Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi (Forensic Bureau).

Inadaiwa kitengo hicho kilibaini mwandiko na saini katika fomu hiyo si za marehemu Tarasila Oisso, aliyekuwa mfanyakazi wa shirika hilo.

Kufuatia matokeo hayo, MDH ilipeleka shauri Mahakama Kuu ili iamue usahihi wa fomu na uhalali wake.

Inadaiwa katika fomu hiyo ya madai kwamba, uchunguzi wa kitengo hicho cha Jeshi la Polisi kilibaini fomu hiyo ilighushiwa Disemba 16, 2022, jambo linalodaiwa kumsukuma mwajiri kuamua kufungua shauri la kuingiliana (interpleader suit).

MDH pamoja na dalali wa bima hiyo walifungua shauri hilo dhidi ya Tsere na Edwald ili mahakama iamue nani anastahili kulipwa bima hiyo ya maisha na kwa kiwango gani. Mfamasia huyo (Tarsila) alifariki dunia Disemba 21, 2022.

Katika fomu hiyo ya madai iliyoko mahakamani, inadaiwa kuwa fomu ya mgawanyo wa bima ya maisha ya Tarsila ilighushiwa wakati ambao mfamasia huyo alikuwa katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) cha moja ya hospitali kubwa jijini Dar es Salaam ambako alikuwa anapata matibabu ya maradhi yaliyokuwa yanamsumbua.

Shauri hilo linatarajiwa kutajwa mbele ya Jaji Hamidu Mwanga Juni 25 mwaka huu, yaani Jumanne ijayo. Wadaiwa wanatakiwa wawe wameshawasilisha majibu ya hoja za walalamikaji.

# Bil. 1.2/- za mradi wa maji zapeleka kicheko Ngara

**Na Judith Julius,** NGARA

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Julius, ameshukuru serikali kutoa Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya mradi wa maji katika Kata ya Nyamiaga, wilayani mwake.

Kanali Julius alitoa shukrani hizo juzi alipotembelea mradi huo, akisema utanufaisha wananchi wa kata hiyo na maeneo jirani.

Alisema serikali imehakikisha huduma nyingine zote kama afya, umeme, barabara na elimu zinapatikana ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, zaidi ya Sh. bilioni 65 zimetolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Wilaya hiyo haikuwa na hospitali ya wilaya.

Diwani wa Nyamiaga, James Eustace, miongoni mwa viongozi waliokuwapo katika ziara hiyo, alishukuru serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa katika Shule ya Sekondari Mumiterama pamoja na madarasa sita ya Shule ya Msingi Kumuyange.

Adelina Didas, mkazi wa Ngara, alisema wananchi wa Kata ya Nyamiaga wanaishukuru serikali kwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapata huduma ya maji karibu na makazi yao.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwenye account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian




Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo ya Wajasiriamali, Dk. Donath Olomi akiwasilisha matokeo ya utafiti wake kuhusu utitiri wa tozo nchini kwa wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Utafiti: Utitiri huu wa tozo ni hatari kibiashara, uwekezaji

**Na Halfani Chusi**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI) limesema kuwapo utitiri wa tozo katika kila mkoa na halmashauri kumekuwa kikwazo katika ustawi wa biashara na uwekezaji nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirikisho hilo, Leodegar Tenga alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salama wakati wa warsha ya kuwajengea uwezo wadau wa sekta ya viwanda vya chakula na vinywaji kupitia.

Katika warsha hiyo, pia kuliwasilishwa taarifa ya utafiti uliofanywa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo ya Wajasiriamali, Dk. Donath Olomi.

Utafiti huo uliofanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro uliangazia namna tozo hizo zilivyo kikwazo kwa wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali nchini.

Tenga alisema Dk. Olomi ni mtafiti msomi na ameainisha vitu vingi ikiwamo mapendekezo ya kufuata kuondoa vikwazo hivyo, akisisitiza kuwa lengo ni kuwapa nafasi nzuri wafanyabiashara wakubwa wanaotamani kuja kuwekeza nchini.

Tenga alisema utofauti wa tozo una athari kibiashara ikiwamo kuongezeka bei za bidhaa na hivyo kusababisha mlaji kununua bidhaa ya bei ndogo kwa gharama kubwa.

"Kwa mfano, mtu amevuna mazao yake Mbeya, ili aje kuuza Dar es Salaam kwenye soko kubwa, atalazimika kusafirisha. Hivi sasa anatozwa huko, akifika Iringa anatozwa tena, njiani pia hivyohivyo anakutana na tozo nyingine, akifika Dar es Salaam nako anakutana na tozo nyingine," alisema.

"Tunataka huyu mfanyabiashara akishatozwa Mbeya, asitozwe tena sehemu nyingine, tunapaswa tuwe na utaratibu ambao utatambua kama ameshatozwa, hatujafanikiwa kuondoa vikwazo.

"Tusipofanya hivyo tunawakwamisha hawa wafanyabiashara au watafanya ujanja wa kutoa rushwa njiani ili kupunguza hizo tozo," alisema Tenga.

Dk. Olomi alisema kutokana na utafiti aliofanya, anapendekeza kuwe na uwazi kuhusu tozo hizo, akifafanua kwamba katika halmashauri karibu zote, tozo hizo hazijatangazwa mahali popote, hivyo mwekezaji anayetaka kuwekeza hawezi kujua viwango vya tozo na kama viko kwa mujibu wa sheria au la.

Msomi huyo pia anapendekeza serikali iangalie namna ya kuondoa tozo zinazokinzana na kujirudiarudia kwenye mikoa na halmashauri nchini, akitolea mfano kwamba mtu akiingiza lori mjini (Kariakoo) kwa ajili ya kupakia au kuondoa bidhaa atakutana na tozo ya maegesho.

Alisema lori hilo pia litatozwa malipo ya kuingia katikati ya jiji na wakati mwingine haijulikani wapi ni mwisho wa kulipia, hivyo kuna maeneo kama hayo yanahitaji marekebisho.

Alisema mkanganyiko mwingine ni tozo zinazotozwa na halmashauri na nyingine Serikali Kuu.

"Kwa mfano, tozo ya kupima afya kwenye viwanda unatozwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) lakini Mamlaka za Serikali za Mitaa (halmashauri) kiutaratibu zinatofautiana.

"Kama unapima magonjwa yanayoambukizwa unapimwa na halmashauri na yale yasiyoambukiza unapimwa na OSHA na tozo wanayotoza kwa mtu mmoja ni Sh. 70,000. Sasa, ukiangalia hii haijakaa sawa.

"Hizi tozo zisiwapo, zinakomoa wenye viwanda. Zitumike kuweka mazingira mazuri. Kuna changamoto za aina hiyo," alisema Dk. Olomi

Mhandisi wa Viwanda Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Karoline Varelian alisema serikali inachukua mapendekezo ya wadau hao, itayachambua na kuyafanyia kazi ili kuweka mazingira rafiki kwao.

Alisema tayari wizara imeshaanza kuzifanyia marekebisho baadhi ya sera na sheria. Watafanyia kazi haraka mapendekezo yaliyotolewa na wadau ili kuondoa malalamiko ya wenye viwanda.

Alisema tozo zimekuwa nyingi na kuahidi kuwa watapitia ushauri uliotolewa kupitia utafiti uliofanywa na Dk. Olomi ili kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara hususani wenye viwanda vya chakula na vinywaji.

## Hospitali, shule zapigwa jeki vifaa vya mamilioni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali kuimarisha huduma mbalimbali za kijamii, Benki ya NMB imetoa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 44 katika sekta za afya na elimu mkoani Shinyanga na Dar es Salaam.

Katika sekta ya afya, benki hiyo imetoa vifaa vya kutolea huduma za afya vyenye thamani ya Sh. milioni 24 katika Hospitali ya Dk. Jakaya Mrisho Kikwete (Hospitali ya Wilaya ya Kishapu) pamoja na zahanati mbili za Busongo na Ng'wanhalanga zilizopo ndani ya Mkoa wa Shinyanga.

Kwenye sekta ya elimu, benki hiyo imetoa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh, milioni 20 kwa ajili ya wanafunzi na walimu wa Shule za Msingi Karakata na Bangulo zilizoko Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

Vifaa vya afya vilivyotolewa ni vitanda vitatu vya kubebea wagonjwa, vitanda 12 vya kujifungulia, vitanda sita vya uchunguzi, magodoro 14 na vitanda 14 vya kulalia wagonjwa.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Seka Urio alisema afya na elimu ni kati ya sekta za kipaumbele kwa NMB, ambayo imekuwa inatumia asilimia moja ya faida yake kusaidia utatuzi wa changamoto katika jamii.

"Changamoto za afya na elimu kwa benki yetu ni jambo la kipaumbele na hii ni kutokana na ukweli kwamba nyanja hizo ndio msingi wa maendeleo ya taifa lolote, ndio maana sisi hutenga asilimia moja ya faida yetu kila mwaka kusaidia sekta hizo pamoja na majanga," alisema.

Baada ya kupokea vifaa hivyo, Mkuu wa Mkoa, Macha alipongeza benki hiyo, akiitaja ni mfano wa kuigwa kwenye sekta binafsi kwa jinsi inavyounga mkono juhudi za serikali katika kuboresha huduma kwa jamii.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Faustine Mlyutu, alishukuru benki hiyo kusaidia sekta ya afya katika mkoa huo, ikiwamo mapambano dhidi ya ugonjwa wa kipindupindu.

Vifaa vilivyotolewa kwa ajili ya shule za msingi za jijini Dar es Salaam ni pamoja na madawati 125, viti 50 na meza 50 kwa ajili ya shule zote mbili. Vilikabidhiwa na Meneja wa Benki hiyo Tawi la Airport, Restus Assenga.

Assenga alisema utatuzi wa changamoto za sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele vya NMB, ambayo hutenga asilimia moja ya faida baada ya kodi ya kila mwaka kusaidia utatuzi wake kama inavyofanya katika afya na kukabiliana na majanga.

"Tunatambua juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kufanikisha utoaji elimu bora na bure mijini na vijijini, nasi kama wadau tunajiona tunao wajibu wa kuunga mkono hilo, ndio maana benki yetu hutenga asilimia moja ya faida yetu kurejesha kwa jamii," alisema Assenga.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya serikali, Ofisa Tawala Mkuu Wilaya ya Ilala, Flora Mgonja alishukuru benki hiyo kwa kutoa vifaa hivyo, huku akisisitiza walimu na wanafunzi kuhakikisha wanavitunza.



Katibu Mkuu wa Kanisa la Waadventista Wasabato Ulimwenguni, Mchungaji Erton Kohler (katikati), akisalimiana na baadhi ya viongozi mbalimbali wa Kanisa hilo nchini, alipofika katika Kanisa la Wasabato Mwembechai, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

UHABA WA SUKARI

# 'Sheria ifumuliwe, vigogo wabanwe'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Tandahimba (CCM), Katani Katani amesema mabadiliko ya sheria ya sukari ndiyo mwarobaini wa tatizo uhaba wa sukari ambalo nchi imepitia kwa zaidi ya miaka 20.

Amesema nchi imepita katika shida hiyo kutokana na waliopewa dhamana kuzalisha, kuagiza na kuuza bidhaa hiyo nchini kupandisha bei kiholela.

Katani aliyasema hayo jana bungeni wakati akichangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema umefika wakati sasa kuwasilishwa bungeni muswada wa sheria ili kufanyiwa marekebisho sheria na kukomesha, hali hiyo ambayo kila mwaka wabunge wamekuwa wakisimama bungeni kulalamika bei ya sukari.

"Hatuwezi kuendeshwa na watu saba kutupangia bei ya sukari Watanzania takribani Sh. milioni 61 tunaomba hiyo sheria ije bungeni hapa, ili tukomesha hali hii kwani hiki kikundi cha watu saba hakiwezi kutuendesha sisi ni sawa na mkia uendeshe mwili, hiki ndicho kinafanyika," alisema.

Aliwataka wabunge wenzake kuunga mkono wazo la kuleta sheria ya sukari bungeni, ili ifanyiwe maboresho na kuondoa adha ya bei juu ya sukari ambayo imekuwa ikitokea kila mwaka.

"Leo hii nitashangaa kuona mbunge ambaye atapinga kuletwa sheria hii bungeni, ili wananchi wetu waendelee kupata shida kila mwaka ya kupanda kwa bei ya sukari," alisema.

Alisema serikali imekuwa inatoa vibali kwa ajili ya kuwapa watu wenye dhamana ya kuagiza sukari kutoka nje, lakini hawafanyi hivyo na wakati mwingine wanauza vibali hivyo kwa watu wengine.

"Sukari inapouzwa kilo moja Sh. 6,000, inapouzwa Sh. 7,000, sukari ikauzwa kwa Sh. 5,000, serikali ikaingilia kati kwa ajili ya wananchi wa Tanzania wapate sukari kwa bei nafuu, akapatikana mtu katika kutetea watu ambao kwenye taifa hili ndiyo wanafanya njama wengine tunao ushahidi tunaweza kukupa ushahidi ukiutaka.

"Nikupe mfano, Mweshimiwa Mwenyekiti, sukari inayouzwa nchini, mkulima wa miwa anayelima miwa Kagera na mkulima wa miwa anayelima miwa Kilombero bei ya tani moja ya miwa Kilombero na Kagera ni tofauti, lakini bei ya sukari ni ilele wanayoipanga," alisema.

Mbunge Katani alisema inashangaza kuona kwenye ukanda wa mikoa ya kati wakala wa kuuza sukari ni mmoja ambaye yuko Dodoma.

"Manyara hakuna wakala wa kuuza sukari, pana jambo gani hapa? Haiwezekani katika taifa hili watu saba waweze kutuendesha) Watanzania milioni 61.

"Mweshimiwa (Dk.) Mwigulu Nchemba (Waziri wa Fedha) na Waziri wa Kilimo (Hussein Bashe), mimi niwape matumaini, Watanzania wana akili na wanaona nia ya serikali ya Dk. Samia, wanaona kinachofanywa na serikali isingewezekana muda wote tunakaa bungeni hapa kila mwaka bei ya sukari inapanda, serikali ikawa kimya, ikichukua hatua kunaibuka maneno chungu nzima," alisema.

Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga, alisema mabadailiko ya sheria ya sukari yatasaidia kuondoa tabia iliyojengeka kwa wale walipewa dhamana kufanya mambo kwa maslahi yao binafsi.

"Serikali ilitoa mamlaka kwa hawa watu kwa nia njema, lakini wao hawafanyi kwa maslahi ya umma wanapewa vibali haagizi sukari, wanaficha vibali mfukoni na wengine vibali vile wanaviuza ili sukari ipande bei sukari ni usalama wa taifa watu hao walipewa vibali waagize tani 15,000 wakaleta tani 2,300 ndani ya miezi sita hakuna sukari nchini ili bei ipande," alisema.

**MAFAO**

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Alice Kaijage alishauri mifuko ya pensheni kuanza kufanya biashara badala ya kufanya uwekezaji kwenye majengo na mambo mengine, hali ambayo imekuwa inachangia kwa kiasi kikubwa kupata hasara.

Alisema kuwa hivi sasa uwekezaji wa mifuko mingi ya pensheni umekuwa wa hasara na kusababisha mingi kushindwa kumudu ongezeko la madai ya mafao ya wastaafu.

"Ninashauri mifuko hii kuanza kufanya biashara kama ya mafuta kwani wanachotaka wastaafu wetu ni usalama wa fedha zao, lakini huku kwenye uwekezaji majengo mifuko mingi imeshindwa, angalau kwenye uwekezaji wa hati fungani wamepata faida ya asilimia 75," alisema mbunge huyo.

# Majaliwa: Tutayaenzi mema ya RAS Nzunda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali na Watanzania wataendelea kumkumbuka na kuyaenzi mema yote yaliyofanywa na aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipokwenda kuhani msiba wa Dk. Nzunda, nyumbani kwa marehemu huko Goba, wilayani Ubungo, Dar es Salaam. Dk. Nzunda alifariki dunia Juni 18 mwaka huu kwa ajali ya gari.

"Tuna jukumu la la kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu Nzunda pahala pema, pia tuna jukumu la kuipa faraja familia yake," Waziri Mkuu alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawa za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa alisema kuwa uwezo aliokuwa nao Dk. Nzunda ulikuwa wa aina yake na ni pigo kutokana na kazi kubwa aliyokuwa anaifanya.

Waziri Mchengerwa alisema kuwa vijana wengi walijifunza kutoka kwake, akisisitiza, "Tuna mengi ya kusema kama ushuhuda wa yale aliyoyafanya katika kipindi chote cha uongozi wake."

Awali mtoto wa marehemu, Victor Nzunda, alisema baba yao aliwaasa waishi maisha ya kufanya ibada, akisisitiza kuwa, "Baba yetu alikuwa mcha Mungu".

Victor alisema baba yao alikuwa akiunganisha watu wenye mahitaji, wakiwamo yatima na wazee pamoja na kwenda hospitalini kwa ajili ya kufariji wagonjwa.

# TRC yakamilisha upembuzi reli ya Mtwara-Mbambabay

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limekamilisha upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Mtwara-Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma (Km 1,000).

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alibainisha hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Jacqueline Msongezi, aliyetaka kujua lini serikali itaanza ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay.

Kihenzile alisema serikali kupitia TRC imekamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli ya Mtwara-Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma.

Alisema kuwa hivi sasa serikali inaendelea na utafutaji rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji mradi huo kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

"Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/25, kiasi cha Sh. milioni 702.6 kimetegwa kwa ajili ya kumwajiri mshauri elekezi atakayekuwa na jukumu la kuandaa andiko, makabrasha ya zabuni na kutusaidia kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi.

"Ninaomba kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongezi, pamoja na wananchi wa Mtwara na Ruvuma kuwa na subira wakati serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa njia hii kwa kiwango cha 'standard gauge'," alisema Kihenzile.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji epukeni migogoro kusajiliwa timu zaidi ya moja

**WAKATI** wachezaji wanaotarajia kushiriki msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Kuu ya Wanawake na ligi nyingine zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), wakiwa wamepumzika, tayari dirisha la usajili limeshafunguliwa.

TFF ilitangaza dirisha la usajili lilifunguliwa tangu Juni 15, mwaka huu, hivyo huu ni wakati rasmi wa wachezaji na viongozi kufanya mazungumzo kuhusiana na usajili ikiwa ni maandalizi ya awali kuelekea msimu mpya wa mashindano ambayo utaanza ifikapo Agosti.

Lakini kama vile bado mchakato huu kwetu unaonekana mpya, kila mwaka hatutaacha kusikia migogoro na mivutano kati ya klabu na wachezaji.

Migogoro huanzia baadhi ya klabu kutangaza bado inammiliki mchezaji fulani na mchezaji huyo husika anayetajwa kusikika hadharani akikanusha yeye hana mkataba na timu iliyomtaja, akisema alishamaliza mkataba wa awali.

Lakini pia wakati mwingine tumesikia klabu au mchezaji akitangaza taarifa ambazo si sahihi, bila kujua athari zake za baadaye, maana hapo kuna kosa la udanganyifu au kwa kutokujua kwa sababu mikataba mingi huandikwa kwa lugha ya kigeni ya kingereza.

Kwa upande wa wachezaji wetu wa Kitanzania wanaokwenda kutafuta riziki nje ya nchi wao hukutana na baadhi ya mikataba imeandikwa kwa lugha ya kifaransa huku bahati mbaya anasaini peke yake bila meneja au wakala na kujikuta amekubali kuweka saini au dole gumba katika mkataba wa muda mrefu, lakini maslahi finyu.

Hizi zama zimekwisha, tunatakiwa tufanye mchakato huu kwa weledi zaidi, ni aibu nchi ambayo ligi yake iko katika nafasi ya juu kwa ubora barani Afrika bado utasikia kuna kesi kuhusiana na kusajili wachezaji bila kufuata taratibu.

Kama ambavyo tumejifunza vitu vizuri kwa nchi zilizoendelea, umefika wakati michakato hii ya kusajili wachezaji ikawekwa wazi na klabu inayotaka kununua au kuvunja mkataba wa nyota ikafahamu taratibu anazotakiwa kuzifuata bila kufanya makandokando ya aina yoyote.

Ni aibu kwa klabu kubwa kama Simba kuanza kugombania mchezaji hadharani wakidaiwa kutotimiza masharti waliyopewa wakati wa kukamilisha usajili wa beki wa kati, Lameck Lawi.

Simba inadai ilipaswa kumpata mchezaji huyo ili kufanya vipimo vya afya kabla ya kukamilisha kiasi cha mwisho cha malipo ya uhamisho wake, nyota huyo alikosekana kwa sababu ya kuwa miongoni mwa wachezaji wa Taifa Stars waliokuwa Indonesia katika mechi za kirafiki za kimataifa, hivyo mchakato wa vipimo ulikwama.

Hata hivyo Simba ilikamilisha sehemu ya pili ya fedha walizotakiwa kulipa, lakini inashangaza Coastal Union ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), Steven Mnguto, kueleza beki huyo bado ni mchezaji wao halali.

Tumeshuhudia migogoro ya namna hii baadhi 'ikiwapoteza' wachezaji husika na kushindwa kuonyesha kiwango chake halisi kwa sababu muda wa maandalizi ya kujiandaa na msimu mpya ambao nyota wengine huanza mazoezi au husafiri kwenda ughaibuni, yeye hubakia nyumbani ili kusubiria hatima ya kesi yake.

Na shauri lake linapofanyiwa kazi, hujikuta baadhi ya wachezaji wanaangukia katika kikosi ambacho hakiko 'moyoni' kwake au anatua kwenye timu ambayo hapati namba na hali hiyo humvuruga na kuufanya msimu mkwake kuwa mchungu.

Huu ni wakati wa uwazi, teknolojia, klabu zifanye usajili wa wachezaji kwa kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa, klabu zisione dhambi pia kutoa ushirikiano kwa timu zinazohitaji kununua jumla au kwa mkopo wachezaji na kufanya zoezi hili kama biashara haramu, hupelekea kuzima ndoto za wachezaji wetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Uhakiki umiliki wa klabu Ligi Kuu nchini uzingatie weledi

**NI** kweli kabisa zipo taarifa katika Ligi Kuu Tanzania Bara zipo taasisi zinazomiliki zaidi ya klabu moja kwa namna moja ama nyingine.

Ingawa siyo dhahiri, lakini dalili, tetesi, malalamiko, manung'uniko na hata ukiunganisha 'doti' utagundua kuna kitu kama hicho, hasa kwa msimu miwili iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Awali ilikuwapo tena dhahiri, lakini Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), lilisimama kidete na kumaliza kitu hicho.

Hata hivyo, yale ambayo yaliyokataliwa na TFF wakati huo kwa kupewa mwongozo na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), yamerejea tena.

Zamani kulikuwa na timu za majeshi zaidi ya moja katika ligi hiyo ya juu nchini, lakini ukaja mwongozo ambao ulitaka kila taasisi iwe na moja tu.

Kulikuwa na Polisi Morogoro na Polisi Dodoma zinazomilikiwa na Jeshi la Polisi Tanzania chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, ambazo zote kuna wakati zilikuwa zinashiriki Ligi Kuu.

Kulikuwa na JKT Ruvu, Mgambo Shooting na Ruvu Shooting ambazo zote zilikuwa zinamilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Athari ya timu hizi ni endapo kama klabu moja inahitaji pointi tatu ili iwe bingwa, au isishuke daraja, halafu moja kati ya mechi yake inacheza dhidi ya 'wanandugu', haiwezi kuzikosa.

Haiwezekani Ruvu Shooting ikose pointi tatu kutoka kwa JKT Ruvu kama inazihitaji ili isishuke wakati zote zinamilikiwa na taasisi moja, na mwajiri wao ni huyo huyo kasoro mikoa tu ndiyo tofauti.

Uongozi wa Rais, Leodegar Tenga, uliondoa kadhia hiyo, na ndiyo maana unaona leo kuna timu moja tu ya Jeshi la Polisi inaitwa, Polisi Tanzania, na Jeshi la Kujenga Taifa ikabaki na JKT Tanzania tu. Jeshi la Magereza wao waliliona hilo tangu zamani, wakawa na timu yao moja iliyobeba sura ya kitaifa, Prisons.

Naona kama sasa tunarudi nyuma. Kuna ujanja unafanyika, baadhi ya watu wanamiliki zaidi ya timu moja 'kiujanja ujanja' ambapo Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, amesema ni ngumu kuwabaini, lakini watalishughulikia.

"Hili la ndani ya ligi kuna mtu anamiliki zaidi ya klabu moja, tabu tunayoipata ukienda kwenye hati ya umiliki huioni, na huwezi kumpata na sisi tunafanya kazi kwa nyaraka siyo hisia, kisheria wanakushinda, lakini hili limezua mjadala mkubwa, sasa kuthibitisha ndiyo changamoto, lakini siyo wenzetu wa Idara ya Sheria wameiacha iendelee, hapana, bado wanatafuta namna ya kupambana nalo, ikiwamo kufuatiliwa mwenendo wao wa kifedha ya klabu husika na wataalam wa kazi hizo, pamoja na chochote ambacho wataona kinaweza kuwawezesha kutambua mtu mmoja anajihusisha na klabu mbili katika ligi moja," alisema Kasongo.

Nadhani pia wangeenda mbali zaidi hata baadhi ya makampuni ambayo yamewekeza katika klabu moja, halafu yanakwenda kudhamini timu zingine, hii si sawa hata kidogo.

Ulaya wamekataza vitu kama hivi, kampuni kama ina maslahi na klabu moja, hawezi kumiliki, au kudhamini nyingine kwenye ligi hiyo hiyo kuwepa upangaji wa matokeo. Kama hata wenzetu wanaogopa suala hilo na wanajua kuna uwezekano wa kuwepo, sisi ni nani tusiwe na tahadhari?

Naipongeza Bodi ya Ligi kwa kuamua kuvalia njuga masuala hayo, ambayo yanaweza kuifanya ligi yetu isiaminike mbele ya mashabiki na jamii ya wapenda soka kwa ujumla.

Napongeza pia ahadi ya Bodi ya Ligi kuahidi kuweka kanuni ya kuzuia timu kuhamahama mikoa kwa msimu mmoja wakati ligi inaendelea.

Hili tumeliona kwa Singida Fountain Gate, iliyohama kutoka mkoani Singida na kuhamia jijini Mwanza, huku Ihefu ikitoka Mbarali, Mbeya kutumia Uwanja wa CCM Liti ulioko Singida.

Tunahitaji Ligi Bora isiyo na mikanganyiko na maswali tele kwa wadau ambayo yataifanya isiaminike.

# RC: Tusishangilie hati safi, tujikite matumizi yenye tija

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amesema halmashauri za mkoa huo hazipaswi kushangilia kupata hati safi badala yake zijikite kwenye matumizi yenye tija.

Kunenge alielekeza hayo jana wakati wa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Mkuranga kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kilichofanyika mjini hapa.

Alisema halmashauri za mkoa huo zimekuwa zinapata hati safi kila mara, jambo ambalo kwa sasa limekuwa la kawaida, hivyo wanapaswa kujikita kwenye matumizi yenye tija kwa kuangalia vipaumbele.

Alisema wananchi wanataka kuona hali halisi kwenye maisha yao ya kila siku na siyo kwenye karatasi.

Kunenge alisema kuanzia mwaka ujao, kila mkuu wa idara awajibike na hoja zake mwenyewe na kwa utaratibu huo utasaidia kutokuwa na hoja katika vipindi vijavyo.

Mkuu wa Mkoa pia alielekeza halmashauri hiyo kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuongeza umahiri wa kukusanya na kuwa makini kwenye matumizi kwa kutekeleza miradi yenye yenye tija.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Rashid Mchata alipongeza halmashauri hiyo kwa kufanya vizuri kwenye ukusanyaji mapato huku akisisitiza uibuaji vyanzo vipya vya mapato.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Nassir alitoa rai kwa watumishi kuwa waadilifu na kila mkuu wa idara akae na wataalamu wake kujadili mikakati ya kuinua mapato.

Nassir pia alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Waziri Kombo kukaa na timu yake kuhakikisha fedha zinazotengwa zinakwenda kujibu hoja za wananchi ambao ndio walengwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mohamed Mwela alisema wamepokea maagizo yaliyotolewa na yafanyiwa kazi.

Awali Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kombo alisema hoja za CAG dhidi yao zilikuwa 49. Hadi sasa, hoja 31 zimefungwa 31. Hoja 18 zilizobaki wanaendelea kuzifanyia kazi



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa pili kushoto), akiangalia mashine ya kutolea risiti ya mfanyabiashara Ali Salm (kulia) wakati wa operesheni maalum ya kutokomeza bidhaa feki na kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi, iliyofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja wa Mamlaka hiyo, Wilaya ya Kinondoni, Dickson Qamara na Meneja Msaidizi, Alex Mwakarobo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Fisi aua mtoto mgongoni mwa mama

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

MTOTO mwenye umri wa miezi minane, Luka Michael, mkazi wa Kijiji cha Orkirungrung, Kata ya Endonyongijape, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, ameuawa na fisi akiwa amebebwa mgongoni na mama yake.

Kabla ya kumuua mtoto huyo na kumjeruhi Namayani Michael ambaye ni mama wa mtoto huyo, fisi huyo aliwajeruhi watu wengine watano wakazi wa Kijiji cha Irkuji, kuua na kujeruhi mifugo.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi wa mkoani hapa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, George Katabazi, alisema matukio hayo yalitokea juzi (Juni 20) kati ya saa saba usiku na saa 12 alfajiri.

Kamanda Katabazi alisema fisi huyo aliuawa baadaye na wakazi wa eneo hilo. Majehuhi wamelazwa Hospitali ya Wilaya ya Simanjiro wakiendelea kupatiwa matibabu.

Akifafanua zaidi kuhusu tukio la mauaji ya mtoto huyo, Kamanda Katabazi, alisema alfajiri ya kuamkia Juni 20, mwaka huu, mama huyo akiwa na mtoto wake mgongoni akienda kuchota maji, alikutana na fisi ambaye alimvuta mtoto na kumng'ata mkononi na maeneo mbalimbali ya mwili wake.

"Mama huyo alijitahidi kumnusuru mwanawe, lakini hakuweza kwa kuwa naye alijeruhiwa na fisi huyo, akamuua mtoto; na hata watu wengine walipojitokeza kutoa msaada walikuwa wameshachelewa," alisema.

Kamanda Katabazi alisema fisi huyo kabla ya tukio la kuua, alivamia mifugo na kuua mbuzi wanne ambao ni mali ya mfugaji, Papa Daniel.

Pia alimjeruhi maeneo mbalimbali ya mwili mfugaji huyo na mtoto wake, Nginji Daniel.

Alisema fisi huyo alijeruhi watu sita na kuua kondoo 11, mbuzi wawili na kujeruhi ng'ombe 12.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alipofika katika vijiji hivyo kutoa pole alisema" "Nimefika kwa haraka kuwajulia hali na kuwapa pole waathirika wote waliokutwa na tukio hili, nimeagiza gharama zote za matibabu za waathirika zibebwe na serikali na mkono wa rambirambi kwa familia iliyopoteza mototo."

Mkuu wa Mkoa pia alielekeza Idara ya Maliasili kufuatilia na kushughulikia wanyamapori hao wanaovamia maeneo ya makazi ya watu ili matukio kama hayo yasijitokeze.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauari ya Wilaya ya Simanjiro, Jacob Kimeso, ambaye ni Diwani wa Kata ya Edonyongijape, alisema mama mzazi wa mtoto huyo aliyefariki dunia, Namayani Michael, yuko hospitalini akiendelea na matibabu kutokana na kujeruhiwa na fisi huyo.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



HABARI KITAIFA



Wajumbe wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakiangalia uzalishaji umeme kwenye Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP), walipotembelea mradi huo, wilayani Rufiji, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mradi Bomba la Mafuta Ghafi waboresha maisha ya wanavijiji

**Na Rodgers Kidesi**

MRADI wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatajwa kubadilisha maisha ya wananchi zaidi ya 9,000 walioguswa pamoja na jamiii iliyo katika maeneo yaliyopitiwa na mradi huo.

Ofisa Mawasiliano wa Mradi huo, Abass Abraham amesema umeacha alama chanya ya maendeleo na uchumi ambayo haitosahaulika kwa jamii husika.

Abraham alikuwa anazungumza na waandishi wa habari katika warsha iliyofanyika jijini Dar es Salaam kuelezea maendeleo ya mradi huo.

Alibainisha kuwa hadi sasa wananchi wameshalipa fidia za kupisha mradi huo kwa asilimia 99.

"Tumeshalipa madai ya waguswa zaidi ya asilimia 99, na asilimia chache iliyobakia haijalipwa kwa sababu mbalimbali zikiwamo za kifamilia, kama vile za suala la mirathi baada ya mhusika kufariki dunia kabla ya malipo kutolewa," alisema.

Ofisa huyo alisema kwamba kwa waguswa ambao nyumba zao zimepitiwa na ujenzi wa bomba hilo, walipatiwa uamuzi wa kuchagua ama kulipwa fidia au kujengewa nyumba ambapo jumla ya waguswa 339 wamejengewa nyumba.

"Waguswa 339 walioridhia kujengewa nyumba wameshajengewa nyumba zao za kisasa zenye kutumia nishati ya umeme, tangi la kuhifadhi maji, choo cha kisasa pamoja na jiko la kisasa.

"Kila mguswa alifidiwa nyumba kwa idadi ya vyumba kama aliyokuwa navyo awali, lakini safari hii ni nyumba ya kisasa iliyojengwa kwa teknolojia ya zege kutoka Afrika Kusini," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na nyumba hizo kuwa za kisasa tofauti na nyumba zao za zamani ambazo zilijengwa kwa udongo na hazina umeme, waguswa hao walipatiwa elimu na kitabu cha mwongozo wa matumizi sahihi ya nyumba hizo ili zidumu.

Alisema mbali na fidia za nyumba, waguswa walihakikishiwa upatikanaji chakula salama kwa kugawiwa bila malipo na kuongeza kuwa pia mradi wa EACOP umetoa ajira kwa jamii inayozunguka kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

"Waguswa wa mradi huu pia wamepatiwa elimu ya kilimo ambayo imewasaidia kulima kisasa na kupata mavuno mengi na bora, hali ambayo imesaidia katika kuwabadilishia maisha yao kwa kupata kipato zaidi kutokana na kilimo," alisema.

Ofisa huyo alisema mradi pia umesaidia kuvinyanyua vikundi vidogo vya biashara katika maeneo yaliyoguswa, umejenga na kukarabati madarasa ya shule, umegawa madawati, umejenga barabara kwa kiwango cha changarawe na kupanua miondombinu ya maji katika eneo la Tanga.

Kuhusu maandalizi ya awali, ofisa huyo alisema wameshafanya kwa kuchukua maeneo ya kujenga kambi na ujenzi umeshaanza.

"Kwa upande wa uwekaji mabomba, wataalamu wanasema kuwa ni jambo rahisi, kwa sasa tayari uzalishaji mabomba umeshaanza," alisema.

Fatuma Msumi, Mkuu wa Idara ya Uhamasishaji Jamii EACOP, alisema mradi umepita katika mikoa minane, wilaya 25, halmashauri 28, kata 117 na vijiji 233 pamoja na zaidi ya vitongoji zaidi ya 450.

Alisema kwamba tangu mwaka huu uanze, wameonana na wadau wa mradi huo wapatao zaidi ya 24,000 kupitia mikutano ya hadhara, majadiliano mbalimbali waliyofanya na kati ya yao, asilimia 44 ni wanawake.

"Tunapenda zaidi kuchukua takwimu za wanawake ni idadi gani kwa sababu tunajua mila na desturi zetu wanawake mara nyingi hawaendi kwenye mikutano, hivyo sasa tunapoangalia ni idadi gani ya wanawake tunaangalia taarifa hizi zimewafikia makundi gani," alisema Fatuma.

Aliongeza kuwa lengo kuu la kuangalia ushirikishaji makundi yote ya jamii katika mradi huo ni kuhakikisha fursa zinazopojitokeza, makundi yote yanazipata kwa usawa na wanawake na vijana hawaachwi nyuma.

Mradi wa EACOP una urefu wa kilomita 1,443 kutokea Kabale, wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, mkoani Tanga, Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, mradi ni mrefu zaidi ukiwa na kilomita 1,147 na kwa Uganda ni kilomita 296.

# Ajali ya gari lililobeba nyama yaua wanne

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa baada ya gari aina ya Toyota Noah lililokuwa limebeba nyama ya ng'ombe kwa ajili ya sikukuu ya Eid Al Adha kugonga lori kwa nyuma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, akizungumza na waandishi wa habari juzi mjini hapa, alisema ajali hiyo ilitokea Juni 19 mwaka huu saa tatu usiku katika Kijiji cha Kwae, Kata ya Msisi, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, barabara kuu ya Singida - Mwanza.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni gari aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T 674 CSY lililokuwa na abiria wanane na nyama ya go'mbe, kuligonga kwa nyuma lori la mizigo aina ya Mercedes lenye namba T 352 DDP, mali ya kiwanda cha kusindika pamba kilichoko Manispaa ya Singida.

Kamanda Kakwale alisema baada ya Toyota Noah kuligonga lori hilo, gari lingine aina ya Toyota Carina lenye namba za usajiri T 143 TLV lililokuwa linaendeshwa na Elias Zabron ambaye ni Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara nalo iliiligonga Noah kwa nyuma.

Aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Kidanka Ntandu ambaye alikuwa dereva wa Toyota Noah; Ally Ibrahimu (40), mkazi wa mjini Singida; James Muro (45), mkazi wa Makiungu ni mwanaume mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 50 ambaye jina lake halijafahamika.

Alisema miili ya watu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida. Majeruhi wa ajali hiyo ambao wanapatiwa matibabu katika hospitali hiyo ni Omari Jumanne, mkazi wa Singida; Ramadhani Kisuda (36), mkazi wa Singida; Joseph Kim (45), mkazi wa Makiungu na Athuman Salehe (41), mkazi wa Majengo, mjini Singida.

Kamanda Kakwale alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Noah ambaye alikuwa mwendo kasi, kushindwa kulimudu gari lake na hivyo kugonga lori kwa nyuma.

# Mpango atoa maagizo saba sekta ya madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo saba yatakayosaidia kuboresha sekta ya madini nchini, ikiwemo wadau wote wa sekta hiyo kuzingatia, kufuata sheria na kanuni ikiwa ni pamoja na kutotorosha madini ili kuondoa usumbufu na kurahisisha utendaji wa shughuli zao.

Aidha, wachimbaji lazima wahakikishe wanakuwa mstari wa mbele kulipa tozo na ushuru halali ili kusaidia kuongeza mchango wa sekta ya madini katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Dk. Mpango alibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati akifungua kongamano la wiki ya madini lililoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA)

"Wizara ya Madini zishirikisheni na Wizara mnazofanya nazo kazi katika eneo la uchimbaji madini kwa mfano wizara ya ardhi, maliasili na utalii, maji na mazingira kabla ya kutoa leseni kwa wachimba madini, ili kuepuka migogoro na muingiliano wa shughuli nyingine kulingana na matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo husika.

"Mfano hapa Dodoma hapo kwenye kilima cha UDOM eneo la Njedengwa, kuna uchimbaji wa madini ya kokoto unaendelea, hali ambayo inaharibu kabisa mazingira,"alisema Dk. Mpango.

Alisema mwaka juzi niliagiza kilima hicho chote kipandwe miti ili kupendezesha mandhari lakini kuna viongozi wametoa vibali kuchimba kokoto na kifusi.

"Waziri wa madini na waziri wa nchi muungano na mazingira angalieni namna bora ya kuratibu shughuli za uchimbaji madini, ili kuepuka uharibifu wa mazingira katikati ya miji na majiji,"alisema.

Alisema bado kuna wachimbaji wengi wadogo wanafanya shughuli za uchimbaji kwa kubahatisha na kutumia muda mwingi na nguvu kubwa na kuambulia kidogo na wakati mwingine kukosa kabisa.

Alisema kutokana na hali hiyo wizara ya madini lazima iongeze wigo na jitihada za utafiti wa madini kupitia taasisi ya GST, ili kuwaongoza vyema wachimbaji wetu wadogo kutoka kwenye kuchimba kwa kubahatisha.

Alisema serikali imekuwa ikipoteza nguvu kazi kubwa kutokana na vifo vinavyotokea katika migodi mbalimbali.

"Wizara ya madini isimamie sheria na kanuni za uchimbaji bora na salama, ili kuepuka ajali zisizo za lazima zinazopelekea vifo na majeraha kwa wachimbaji wadogo,"alisema.

Alisem ajira na mapato yanapotea kutokana na kutosimamia ipasavyo utaratibu wa kuongeza thamani madini yanayopatika nchini.

Aidha, aliitaka wizara ya madini kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kuhakikisha madini yanayochimbwa yanaongezwa thamani nchini, jambo litakalosaidia upatikanaji wa mapato na ajira kwa Watanzania.

"Wizara na tume ya madini hakikisheni wachimbaji wadogo waliopata leseni za madini na kuwekeza mitaji yao wasinyang'anywe kwa kigezo kuwa walipewa leseni hizo kwenye maeneo ya wachimbaji wakubwa,"alisema.

Dk. Mpango alisema suala lisiloeleweka vizuri ni kumpatia mchimbaji mdogo leseni ya uchimbaji madini na baada ya kuanza uwekezaji ananyang'anywa na mamlaka ile ile iliyompatia.

Alisema hali hiyo inaleta hisia za uwezekano wa uwepo wa mazingira ya rushwa.

Vile vile, alitaka wizara hiyo na tume ya madini kuangalia uwezekano wa kuwataka wachimbaji wakubwa na wa kati wanaochimba madini yenye thamani kubwa kurejesha mchango wao kwa jamii katika maeneo yanayowazunguka.

"Kwa mfano hapa Dodoma katika vijiji vya Asanje, Duluu, Gawaye na Itiso kuna uchimbaji wa madini unaoendelea, lakini wananchi wa maeneo hayo hawanufaiki kabisa na chochote,"alisema.

## Serikali yaridhishwa na tafiti kurahisisha kazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAFITI zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Dodoma kuhusu mambo mbalimbali, zimekuwa msaada kwa serikali katika kupata majawabu ambayo yanarahisisha ufanyaji wa kazi imeelezwa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula alisema hayo juzi wakati akifungua Kongamano la Kimataifa la Sayansi na Teknolojia na Ubunifu lililofanyika jijini Dodoma.

Alisema vyuo vikuu vimefanya kazi ya kufanya tafiti tofauti na kutangaza matokeo hayo kwa jamii yanayosaidia katika usuluhisho wa changamoto.

Alisema kwenye sayansi, ubunifu na teknolojia kuna mambo mapya yanayotokea duniani na Chuo Kikuu Cha Dodoma hakipo nyuma kuendana na mabadiliko hayo.

"Leo wanaonyesha matokeo ya tafiti walizozifanya na jinsi gani wamechangia kwenye jamii ya wasomi, lakini Chuo Kikuu cha Dodoma kina mchango mkubwa sana kwa serikali yetu.

"Kwao nimefika leo kuangalia wanachokifanya, wana maonyesho mazuri, kuna teknolojia wanafanya wamebuni na wanafunzi wanashiriki vizuri na mpango wao mpaka mwaka 2026 kiwe ni chuo namba moja Tanzania ambacho kitakuwa kimetoa machapisho mengi," alisema Rwezimula.

Aidha, alisema tafiti hizo zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Dodoma zimekuwa msaada kwa serikali katika kupata majawabu ambayo yanarahisisha ufanyaji wa kazi.

Kwa upande wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Profesa Lughano Kusiluka alisema mkutano huo wa kwanza umetayarishwa kwa ajili ya kujadili mambo ya sayansi, teknolojia na ubunifu huku ukihudhuriwa na wanasayansi wabunifu kutoka ndani na nje ya nchi.

Kusiluka alisema Chuo Kikuu cha Dodoma kina wataalamu katika idara tofauti, ikiwemo wa mabadiliko ya tabia nchi, jografia pamoja na kitengo kinachofundisha namna ya kupambana na majanga pamoja na wahandisi wa mambo ya mazingira.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (katikati) na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TAMISEMI: Walimu 106,000 kupandishwa madaraja Julai

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

SERIKALI inatarajia kuwapandisha madaraja walimu 106,000 kuanzia Julai mosi mwaka huu. Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde, alisema hayo juzi katika kikao kazi cha kuhamasisha ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani Iramba mkoani Singida.

Dk. Msonde katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Ofisa Elimu Mkoa wa Katavi, Upendo Rweyemamu alisema serikali imedhamiria kutatua malalamiko yote ya kada ya ualimu.

Alisema walimu wote nchini wamekuwa na changamoto zinazofanana ambazo serikali imekusudia kuzitatua zote.

Alieleza baadhi ya changamoto hizo ni kupanda madaraja, kubadilishiwa muundo baada ya kujiendeleza kielimu, madai au mapunjo ya mshahara.

Nyingine ni kulipwa stahiki za likizo, kulipwa stahiki za uhamisho na matumizi ya lugha zinazodaiwa kutokuwa za staha kutoka kwa baadhi ya viongozi.

"Changamoto zote hizi serikali imeamua kuzifanyia kazi na kuziondoa kabisa kwa lengo la kuwaacha walimu wakifanya kazi kwa furaha," alisema.

Pia aliwatoa hofu viongozi hao kwa sababu mambo yameisha anza na yanaendelea kwa lengo la kuhakikisha kila mwalimu nchini hahangaiki tena na habari za madaraja.

"Nimeelekezwa nitamke kwamba ifikapo mwezi Julai 01, 2024 walimu 54,000 watapanda kwa mserereko na walimu 52,000 watapanda kawaida," alithibitisha.

Mbali na hayo aliwataka walimu hao kutimiza haki yao ya kufanya kazi kwa lengo la kupata maboresho wanayoyahitaji husasan katika kipindi hicho ambacho serikali inawahangaikia.

Kwa upande wa Ofisa Elimu Mkoa Singida, Dk. Elipidius Baganda alimuhakikishia kiongozi huyo, yote aliyoyaelekeza watayafanyia kazi. "Niwaombe viongozi wote tukayafanyie kazi tuliyoelekezwa na kuendelea kutembea kifua mbele kwa sababu viongozi wote wametengenezwa na mwalimu, hivyo mwalimu ni mtu mkubwa," alisema.

Aidha, aliwakumbusha kuwa kujitambua huko, alikufanya Hayati Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha Uhuru na Maendeleo (Freedom and Development) ukurasa wa 68 aya ya pili alichokiandika mwaka 1973.

Dk. Baganda alimnukuu Mwalimu Nyerere kuwa unavyoniona nilivyo sikuzaliwa hivi, nipo kama nilivyo kwa sehemu kubwa ya ualimu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Mbelekese wilayani Iramba, Sebastian Gunda alimshukuru kiongozi huyo na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote aliyowapatia.

"Ninaamini siku zimebakia chache kwa sababu tarehe mosi sio mbali, hivyo tumeyapokea maelekezo yako," alisema.

# SMZ yaelekeza nguvu ujenzi wa uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), katika kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiushuru na kufungamanisha sera za biashara kutasaidia kupatikana kwa soko la bidhaa za Tanzania nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa 17 makatibu wakuu wa AfCFTA unaofanyika visiwani Zanzibar.

Mkutano huo unafuatiwa na mkutano ngazi ya mawaziri utakaofanyika Juni 24 - 25, visiwani Zanzibar, ambapo Tanzania ni mwenyekiti wa mikutano ya ngazi zote kwa mwaka 2024.

Aidha, Dk. Abdallah alisema kuwa bainisha kuwa utekelezaji wa AfCFTA nchini kutachangia kuhamasisha ukuaji wa viwanda na kuboresha mazingira ya biashara, ambako kutatoa matokeo chanya kwa kuongeza ajira na kuongeza pato la taifa.

Alisema kutachangia pia kutoa huduma bora za kijamii kwa Watanzania na hatimaye kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025 na Agenda 2063 ya Afrika yenye maendeleo.

Vilevile, alitoa wito kwa Jumuiya za Wafanyabiashara wa Tanzania kuchangamkia fursa za soko la AfCFTA lenye watu zaidi ya Sh.billioni 1.3 kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango vinavyotakiwa zinazoweza kushindana katika soko hilo.

Alisema wakifanikiwa kufanya hivyo watakuwa wanatekeleza kwa vitendo dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua nchi kiuchumi, kibiashara na kiuwekezaji.

"Wenzetu wanakimbia sisi tunatakiwa kukimbia zaidi na ni jukumu letu sasa watanzania kuchangamkia fursa zilizopo katika mkataba wa AfCFTA na hapo ndipo tutakuwa tunatekeleza kwa vitendo, ile dhamira ya Rais Samia katika jitihada zake katika kufungua nchi kiuchumi, kibiashara na kiuwekezaji,"alisema Dk. Abdallah.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Fatma Mabrouk Khamis, aliwataka makatibu wakuu hao wa biashara kuhakikisha wanatimiza malengo ya AfCFTA katika kuunda Afrika yenye ustawi na jumuishi, ili kuhakikisha wananchi wa kila nchi wananufaika na manufaa ya AfCFTA yanagawanywa kwa usawa bila kuacha nchi mwananchama yoyote nyuma.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wote hususani wananwake na vijana wa Tanzania Bara na Visiwani kuchangamkia fursa hizo kwa kuuza bidhaa zenye ubora na zenye asili ya Tanzania kulingana na mahitaji ya soko hilo linalojumisha nchi 54 za Afrika.

Alisema wakichangamkia soko hilo wataongeza ajira kwa kuwa AfCFTA inatoa fursa ya kuuza bidhaa au huduma ndani ya Bara la Afrika, bila vikwazo vyovyote vya kiushuru kwa nchi yoyote Afrika ambayo ni mwanachama.

Akitoa mfano wa bidhaa za mwani zinazotengenezwa kwa wingi Zanzibar, Fatma alisema kutokana na fursa za AfCFTA, bidhaa hizo zinauzwa Uganda, Congo na nchi nyingine za Afrika.

Alisema kampuni zinazosafirisha bidhaa hizo zimepatiwa mafunzo ya kuelewa mahitaji ya soko na kuhakikisha bidhaa zao zinafikia viwango vinavyohitajika.

"Mkataba huu wa AfCFTA unatulazimisha nchi za Afrika kuboresha mazingira ya biashara, kuondoa vikwazo visivyo vya kiushuru, kujenga miundombinu na kuboresha sheria zetu ili kupanua wigo wa soko, kuvutia wafanyabiashara na wawekezaji katika sekta mbalimbali kama vile viwanda, kilimo, mifugo na ufugaji, hali ambayo inaongeza ajira, Pato la Taifa na kukuza uchumi wa wananchi wetu na wa Taifa kwa ujumla," alisema Fatma.

Mkurugenzi wa Huduma za Biashara,Uwekezaji, Haki Mliki Bunifu na Biashara mtandao wa AfCFTA, Emily Ndoria, alisema AfCFTA imetengeneza Itifaki mbalimbali ambazo zinalenga kurahisisha utekelezaji wa AfCFTA na ufanyaji biashara kwa ujumla.

Alisema itifaki hizo zinaziwezesha nchi za Afrika kuuziana bidhaa na huduma baina ya nchi na nchi, kuongeza ajira, pato la taifa na kujitegemea kibiashara na kiuchumi.

Aidha, alizishauri nchi wananchama kuhamasisha wananchi wao hususani wanawake na vijana kutumia fursa zinazopatikana katika mkataba wa AfCFTA kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora na viwango vya kimataifa ili ziweze kukidhi mahitaji na kushindana katika soko hilo muhimu la Afrika.

# Abiria walia upandishaji holela wa nauli

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya madereva na makondakta katika Kituo cha Daladala Makumbusho, mkoani Dar es Salaam, wamedaiwa kupandisha nauli kiholela nyakati za jioni hali ambayo ni kinyume cha sheria na taratibu.

Hatua hiyo imesababisha usumbufu na kuzua malalamiko kwa watumiaji wa usafiri huo, huku wakiziomba kuingilia kati ili nauli iliyopangwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mkazi wa Mbezi Mwisho aliyekuwa kituoni humo akisubiri usafiri, Kelvin Makwinya, alisema kwa maoni yake ni lazima nauli zipande kwasababu muda huo watu ni wengi wanaotaka usafiri na magari ni machache.

Alisema wakati mwingine abiria anakaa kwa zaidi ya saa mbili bila kupata gari, hivyo linapotokea gari lolote inamlazimu kupanda kwa nauli yoyote ili kufika anakokwenda kwa haraka.

Abiria mwingine Ahmad Rashid, alisema foleni ndizo zinasababisha nauli kupanda, hasa ikifika nyakati za usiku, abiria ni wengi lakini magari ni machache kituoni.

"Sasa abiria anaona amekaa muda mrefu kituoni, yale magari ya ruti husika yamechelewa kufika, naye anataka kuwahi nyumbani kwa ajili ya kesho kuwahi kazini, kwahiyo unamkuta anaamua kupanda kwa Sh. 1000, ingawa sio nauli kamili,"alisema Ahmad.

Mfanyakazi wa kujitolea katika kituo hicho, Othman Bonzo, alisema mamlaka husika haitekelezi majukumu yake nyakati za usiku ndio sababu ya nauli kupaa kutokana na uchache wa magari muda huo.

"Hizi gari za chuo, lakini zinaenda Makongo, hakuna gari ya Makongo inayopakia hadi saa mbili za usiku. Njia ya Makongo unakuta kwa siku ina gari moja,"alisema.

Aliyekuwa Mwasisi na Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), Hassan Mchanjama alisema suala la kupandisha nauli kiholela limekuwa changamoto kwa nyakati za usiku, amethibitisha mara kwa mara wamekuwa wakipokea malalamiko kutoka kwa abiria, kuhusu kupanda kwa nauli ikifika usiku, na wamejaribu kushirikiana na mamlaka bega kwa bega kutatua suala hilo.

"Changamoto iliyopo mamlaka kutokufanya kazi usiku ipasavyo, LATRA wametoa leseni kwa muda, kwa mujibu wa kanuni na sheria za LATRA, lakini usimamizi umekuwa changamoto," alisema Mchanjama.

Mchanjama alisema wanaendelea kufanya maboresho ya katiba ndani ya chama, na kubadili jina kuwa Taasisi ya Kutetea Haki za Abiria (Takuha), na kuiomba serikali kuunga mkono jitihada hizo.

Msafirishaji abiria njia ya Posta-Makumbusho, Said Abubakari, alisema wanaopandisha nauli nyakati za usiku ni makondakta na madereva wenye tamaa na kusababisha kuharibu utaratibu uliotolewa na LATRA.

Dereva wa daladala, Idris Abdul alisema changamoto za miundombinu ya barabara husababisha magari kutokufika kwa wakati katika vituo, hivyo abiria wengi hulundikana kwenye vituo.

Aidha, aliiomba serikali kutengeneza miundombinu rafiki kwani wanakaa muda mrefu kwenye foleni, jambo linalosababisha washindwe kufikisha hesabu waliyopangiwa na mabosi zao.

Akizungumzia suala hilo, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa LATRA, Salum Pazzy alithibitisha kuwepo kwa malalamiko ya wasafiri na kwamba ni wajibu wa kila msafirishaji kuzingatia sheria, taratibu za nchi.

Aidha, alisema hatua zilizochukuliwa na LATRA ni kuandika kuhakikisha madereva wanaandika nauli elekezi kwenye ubavu wa gari ili abiria waone, na kwamba wanapaswa kulipa nauli iliyoelekezwa kisheria na sio vinginevyo.

"Tunafanya hivi kuwarahisishia abiria kuweza kufikisha taarifa pale ambapo kuna changamoto na makosa kama hayo, yanapokuwa yamefika, tunafuatilia na tunafanya ukaguzi wetu mara kwa mara, wanaovunja sheria tunawachukulia hatua,"alisema.

Kuhusu wingi na uchache wa magari, alisema: "Kama magari yanakuwa machache kiasi kwamba wanakaa muda mrefu, sasa unajua kila mtu anatafsiri yake, mtu anaweza kukuambia dakika 20 ni muda mrefu, mwingine nusu saa, muda mrefu,"alisema.

Kwa mujibu wa Pazzy, wanaendelea kutoa ushirikiano kwa wadau, huku wakihamasisha na kutoa elimu kupitia vipindi vya runinga, mitandao ya kijamii,maonesho na sehemu mbalimbali, na kwamba ni muhimu wasafirishaji wakajua wajibu wao na abiria kujia haki.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein akisalimiana na watoto wanaosumbuliwa na ugonjwa wa seli mundu, wakati wa maadhimisho ya tatu ya Siku ya Seli Mundu, yaliyofanyika Kikwajuni, Zanzibar juzi. **PICHA: MAELEZO-ZNZ**

# Mtakwimu, wizara kufanya utafiti viashiria vya magonjwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISI ya Mtakwimu mkuu wa Serikali (OCGS), kwa kushirikiana na Wizara ya Afya inajiandaa kufanya utafiti wa hali ya viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza kwa njia ya mawasiliano ya simu, ili kukusanya taarifa kwa wananchi.


Akizungumza na waandishi wa habari Mazizini nje ya mji wa Zanzibar, Mtakwimu wa serikali, Saalum Kassim Ali, alisema utafiti umeshakamilika kwa Tanzania Bara, na kwamba kwa Zanzibar utaanza Juni 23, mwaka huu na kumalizika Julai mwaka huu.

Alisema zoezi hilo litashirikisha watu wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea, likifanikiwa litawezesha kupatikana kwa viashiria muhimu kwa tafiti za baadae kwa muda mfupi bila kutumia gharama kubwa.

Saalum alisema kwamba katika utafiti huo magonjwa yasiyoambukiza maswali yatakayoulizwa yatawezesha kupata matokeo ya msingi kufananisha na matokeo ya awali ya utafiti uliofanyika Septemba 2023.

Aliyataja miongoni mwa maeneo yatakayohusika na utafiti huo ni pamoja na matumizi ya tumbaku, matumizi ya vileo, ulaji wa vyakula mbali mbali, shughuli za mazoezi, masuala yanayohusu kisukari na shinikizo la damu.

Aidha, alisema jumla ya kaya 893 zitahojiwa kwa upande wa Zanzibar miongoni mwa kaya hizo ni pamoja na zile zilizohojiwa wakati wa utafiti wa awali.




## DULLA MAKABILA
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JUNI 22, 2024



# ALIISHI JICHO MOJA

UPASUAJI wa jicho aliofanya msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee, umewashtua watu wengi ambao wameeleza kuwa hawakujua anaishi kwa kuona kutumia jicho moja.

Wiki hii Vanessa alichapisha picha zake mbalimbali katika mitandao ya kijamii akiwa amevaa kifaa maalum katika jicho lake la kulia mara baada ya kufanyiwa upasuaji.

Moja ya video yake fupi alionekana mwanamuziki huyo akicheza na mumewe Rotimi, huku akiwa na kifaa kilicho funika jicho.

"Upasuaji wako wa jicho ukifaulu, Utukufu kwa Mungu," aliandika ujumbe ulioambatana na video hiyo.

Hata hivyo, watu wengi walikuwa hawajui kama mwimbaji huyo wa kibao cha 'No Body But Me' alikuwa haoni jicho moja, hivyo walipata mshtuko baada ya msanii huyo kueleza tatizo hilo lililokuwa la muda mrefu.

"Mimi nilikuwa sioni jicho moja pia, lakini hiyo haijanizuia kufuata ndoto zangu kubwa. Nilipata tatizo lililofanya jicho langu kuwa kipofu. Kwa muda nimekuwa nikitumia jicho moja, jingine ni kipofu," alieleza.

Shukuru Hamisi, alimpongeza msanii huyo kwa kufanya upasuaji huo na kueleza kwamba jinsi alivyokuwa awali hakuna mtu aliyegundua kama alikuwa na tatizo.


"Vanessa alikubali tatizo na kuamua kukaa nalo bila watu kugundua, jambo hili ni la kumpongeza kwa sababu ni nadra mtu kuwa katika hali hiyo bila watu kujua," amesema.

Shabiki mwingine, Grace Lameck, amesema kwamba amejifunza mengi kupitia kwa msanii huyo, kwani licha ya kuonekana kuwa na furaha lakini alikuwa akiumia moyoni kutokana na kuwa na tatizo la kuona.

BT BURUDANI TELE JUMAMOSI JUNI 22, 2024 Nipashe 13

BASI SAWA

## Pablo Lg amkubali Zuchu



MTAYARISHAJI wa muziki anayekuja kwa kasi, Pablo Lg, amesema wimbo wa Hani wa Zuchu, umekuwa kama funguo kwake kwani umempatia mafanikio mengi kisanaa.

Amesema licha ya kumpatia tuzo, wimbo huo umemfanya kujulikana na watu wengi ambao wanampatia kazi nyingi ambazo zimempatia fedha nyingi.

"Nakumbuka nilitaka kutoa kitu kitofauti, ndipo nilipoanza kuweka mapigo ya mchanganyiko wa Amapiano, Zuku na Sebene na hatimaye wimbo wa Hani ulikuwa wa kiwango cha juu na kupendwa na wengi," amesema Pablo Lg.

## Sikuwaza kuimba 'Kibango'



Mwanamuziki wa Bongo Fleva, Lavalava amesema hakuwa na mpango wa kutunga wimbo Kibango, lakini kutoka kwake ilikuwa kama jambo la masihara.

Amesema hata walivyokuwa studio kurekodi hakuwa na wazo lolote, lakini ghafla alijikuta akiimba maneno ya kufurahia bata klabuni na ndipo ukazaliwa wimbo huo.

"Nilikuwa nasema tu huku klabu kuna mademu sana, hapo hapo wenzangu wakaniambia huo ndio wimbo wanaoutaka, ndipo na hapohapo tulianza kurekodi". Amesema Lavalava



# MAKABILA ATAMBIA MAFANIKIO

MWANAMUZIKI wa Singeli, Dula Makabila, amesema kiwango alicho nacho kwa sasa hawezi kufananishwa na wasanii wengine wa muziki huo.

Makabila, amezungumza hayo baada ya hivi karibuni kuwa msanii wa kwanza wa singeli kufikisha wafuasi milioni mbili katika mtandao wa Instagram.

"Huwezi kunifananisha na wanamuziki wengine wa singeli hapa nchini, mafanikio niliyoyapata yanatosha kueleza kwamba nimefanikiwa kuupandisha na kuusambaza muziki wa singeli nje ya mipaka ya nchi yetu," amesema Makabila.



# Akothee apinga kupanda kodi

PAMOJA na wasaniii mbalimbali wa Kenya kuonekana kupinga muswada wa ongezeko la kodi nchini Kenya, Bunge la nchi hiyo limeupitisha kwa wingi.

Mmoja wa wanamuziki waliojitokeza kuupinga ni Esther Akoth, maarufu kama Akothee, ambaye alimtaka Rais William Ruto, aingilie kati kuufuta kwa sababu una athari nyingi kuliko faida.

"Mheshimiwa Rais, wakati unachukua madaraka, presha kwa wananchi ilikuwa tayari imepanda kwa kiwango kikubwa, gharana ya maisha imepanda kiasi kwamba wapiga kura wako wengi wanatatizika kumudu milo mitatu kwa siku, tunaomba zuia," aliandika kabla ya bunge kupitisha muswada huo.

# MASONGI KONKI YA KIHINDI

**Na Adam Fungamwango**

KWA wale vijana au watoto katikati ya miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990, wanakumbuka jinsi kulivyokuwa na filamu nyingi kali za kihindi.

Achilia mbali kile kizazi cha mwanzoni mwa miaka ya 1980, kilichokuwa kikienda Drive Inn Cinema, Odeon, Avalon, ambapo mitaani hakukuwa na video wala televisheni, kulikuja kizazi kingine ambacho tayari video angalau moja moja zilianza kuonekana mitaani.

Badala ya watoto kwenda kwenye majumba ya sinema na ilikuwa kwao ni ngumu kidogo, sasa walianza kwenda kwenye nyumba za watu ambao walikuwa wakionyesha filamu mbalimbali.

Kila mkoa nchini Tanzania kulikuwa na sehemu ambazo watoto walikuwa wakienda filamu.

Dar es Salaam, hasa maeneo ya Kinondoni kulikuwa na sehemu maarufu kama 'Milano' na 'Morocco', karibu kabisa na Kanisa Katoliki Magomeni.

Kwenye filamu za Kihindi, mbali na utamu wa filamu zenyewe, lakini vijana na watoto wanapenda sana nyimbo zake.

Baadhi ya nyimbo za Kihindi zikawa maarufu sana mtaani, na wala haikuwa ajabu kukuta zikiimbwa na vijana na watoto. Wenyewe wakazibatiza jina na kuyaita 'masongi'. Walikuwa na maana ya nyimbo kwa lugha ya kizungu 'songs'.

Hapa leo tutaangalia baadhi ya masongi ya Kihindi yaliyotamba na kupendwa sana enzi hizo.

### Goron Ki na Kalon Ki

Ni moja kati ya 'songi' maarufu sana kwa vijana na watoto wa miaka ile ya 1980 hadi 1990. Sidhani kama kuna aliyekuwa mtoto au kijana licha ya kwamba sasa atakuwa mtu mzima, asiufahamu.

'Goron Ki na Kalon Ki' ni wimbo ambao upo kwenye filamu ya 'Disco Dancer' ambayo staa wa picha alikuwa ni Mithun Chakraborty.

Filamu hii maarufu sana na iliyotokea kupendwa ilitoka mwaka 1882, na ilikuwa na 'masongi' mengi makali 'Goron Ki na Kalon Ki, Duniya Hai Dilwalon Ki.' Hiyo ni sehemu ya wimbo huo.

### Jimmy Jimmy aaja

Hapa sasa ndiyo balaa. Hili 'songi' la Jimmy, ukikuta watoto mtaani wanaliimba utafurahi na roho yako.


Halafu kila mmoja anaujua wimbo huu kikamilifu kwa sababu ni sehemua ambapo staa wa picha Mithun anakwenda kushika gitaa lililotegwa umeme, mama yake atakuja kumuokoa. Filamu ni hiyo hiyo Disco Dancer.

### Juma Chuma Dede

Mwaka 1991 kulitoka filamu moja kati kali ya Kihindi iliitwayo 'Hum'. 'starlingi' wake ni Amitabh Bachchan.

'Juma Chuma Dede' ni moja kati ya 'songi' lililopendwa sana na mashabiki wengi wa picha za kidosi au filamu za Kihindi wakati huo. Na hata hapa nchini bendi ya Varda Arts imesahawahi kuchukua mirindimo ya wimbo huo na kuimba kwa kiswahili.

### Kuch Kuch Hota Hai



'Songi' hili kali lipo kwenye kwenye filamu kali ambayo inaenda kwa jina hilo hilo. Ilitoka mwaka 1998 na kuushtua ulimwengu wa filamu za Kihindi duniani. Staa wa picha hiyo ni Shah Rukh Khan, huku wimbo huo ikitia fora na kupendwa na watu wengi zaidi kuliko wimbo wowote ule kwenye picha hilo.

### My Tarzan

Tarzan ni moja kati ya filamu maarufu mno nchini Tanzania na duniani kote. Ilikuwa ni filamu iliyoonyesha kuwa mapenzi yanaweza kumea popote pale hata pasipo na mbolea, porini na kwa mtu yoyote yule. Ndani yake kuna 'masongi' kibao mazuri, lakini uliokuwa rahisi zaidi kuimbwa na Wabongo uliitwa 'My Tarzan', ambao ulifunika bovu.

FILAMU

# Mke wangu usifanye hivyo




**Na Adam Fungamwango**

"MKE Wangu' ni filamu inayogusia maisha ya ndoa kwa baadhi ya wanawake ambao si waaminifu. Pia inawaonya baadhi ya vijana ambao badala ya kutafuta wasichana ambao 'majimbo yao yapo wazi', wao wanawachukua wake za watu, kitu ambacho kinasababisha migogoro na mitafaruku kwenye ndoa.

Kijana mmoja kwenye mtaa moja, kazi yake ni kuchukua wake za watu. Hali hiyo inasababisha hofu kwa wanaume wengi mtaani hapo. Wakakaa kikao wamfanye nini? Awali walitaka kumuua, lakini wakaogopa vyombo vya sheria. Wakaapa tu kumshikisha adabu, lakini hawakusema nini watamfanya.

Alisi, mke wa Mwamu anarejea asubuhi. Alipolala hapajulikani. Mumewe anajaribu kumwambia kuwa anachofanya si kizuri. Majibu anayojibiwa, ni ya kifedhuli. Mwamu anakwenda kumshtaki mkewe kwa mama yake na kaka yake. Mkwewe na shemeji yake wanajaribu kukaa na Alisi kumuonya, lakini inakuwa ni kazi bure.

Alikuwa na tabia ya kumtoroka mumewe na kwenda kwa hawara yake. Anapoulizwa anasema alikwenda kuinjoi na marafiki zake.

Mwamu anafanikiwa kuwafuma mkewe na hawara yake, anamkanya, lakini jamaa anakuwa mkali kama pilipili.

Siku moja, mama alimkalisha binti yake na kutahadharisha kuwa aliendelea na tabia hiyo ataachwa. Binti anajibu kuwa hawezi kuachwa kwa sababu amemuweka kiganjani mumewe.

Na kweli, Mwamu anampenda mkewe na hayupo radhi kumpoteza. Anaamua kufanya kitu ili kuinusuru ndoa.

Alisi anakwenda kwa hawara yake kama kawaida. Akataka kulala huko huko kama kawaida yake. Ghafla hali yake inabadilika na anazirai. Jamaa hana la kufanya. Maiti ya mke wa mtu ipo ndani mwake. Kwenda polisi akaogopa, akaamua kwenda kwa wazazi wa mwanamke huyo. Kesi ikawa kubwa, na mumewe akaitwa.

Jamaa akaomba radhi sana na kuahidi hatorudia tena tabia hiyo. Kumbe Mwamu, mume wa Alisi, alikuwa amempaka mkewe dawa fulani puani ambayo ukiivuta kwa mda mrefu unazirahi. Baada ya masaa mengi, Alisi alizinduka na kumuomba mumewe msamaha na kuapa hatorudia tena. Amani kwenye ndoa ikarejea.



# Sharon afurahia harusi

MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Sharon Ooja Egwurube, amewashukuru marafiki zake kwa kumuonyesha moyo wa kipekee kwa kumandalia sherehe ya kifahari ya harusi yake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Sharon, ametaja upendo huo hauna kifani na kwamba sherehe hiyo imekuwa bora zaidi nchini Nigeria,

Mastaa mbalimbali walijitokeza kumpongeza akiwamo Beverly Osu, Ini-Dima Okojie, Bisola Aiyeola na marafiki zake wengine.




## Travis alianzisha tena

POLISI nchini Marekani wamemkamata rapa maarufu, Travis Scott, baada ya kuanzisha vurugu ndanui ya boti.

Kulingana na TMZ, polisi wamesema walimtia mbaroni msanii huyo baada ya kuonekana akipigana na watu ndani ya boti hiyo iliyopaki katika fukwe ya Miami.

Taarifa hiyo ilisema, licha ya polisi kumtaka msanii huyo kwenda katika gari lake lilokuwa likimsubiri, alikaidi na kuindia ndani ya boti na kualeta vurugu.


|Travis alikuwa amekunywa pombe wakati wote, kwa hivyo malipo ya ulevi usio na utaratibu yanakuwa mabaya," ilisema taarifa hiyo ya polisi.


## Rema kwa Jollof habanduki

MSTAA wa muziki wa Agroabeats kutoka Nigeria, Rema, amesema hakuna kitu anachokipenda maishani mwake kama kula wali aina ya Jollof.

Jollof ni aina ya chakula unaopikwa na mchanganyiko wa mchele,nyama pamoja na viungo vingi sawa na pilau ya Tanzania.

Hata hivyo, Rema alipotakiwa kuchagua nchi gani kwa Afrika Magaharibi inayoandaa Jollof nzuri, alishindwa kutaja na badala yake alisema kwake chakula hicho hula hata kama kikipikwa Ulaya.



## Kifo cha Stella chaleta simanzi

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nolllywood, Stella Ikwuegbu, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Taarifa ya kifo chake ilitolewa na mtayarishaji wa filamu, Stanley Nwoko, ambaye amesema msanii huyo alikufa juzi kutokana na ugonjwa wa saratani ya mguu.

Kifo chake kimesababisha simanzi na pigo kwa tasnia ya filamu nchini Nigeria, kutokana na kuwa na mchango mkubwa kwa miongo kadhaa.

## Timberlake unawapa wasiwasi wenzio

WASIWASI umewakumba mashabiki wa mwanamuziki mkongwe Justin Timberlake, baada ya hivi karibuni kukamatwa na polisi kwa kosa la kuendesha gari akiwa amelewa.

Kulingana na Newsday, mwimbaji huyo alikamatwa Jumatatu usiku katika eneo la Hamptons jijini New York, baada ya polisi kugundua dereva wa gari hilo hayuko sawa.

Hata hivyo, mashabiki wake walishiriki kumpa pole katika ukurasa wake wa Instagram, huku wengine wakitilia shaka kuhusu matendo yake yanayojitokeza kila mara kwa kuhisi hayuko sawa kisaikolojia.



# Waziri Ummy aagiza kampuni ya MDS kuzalisha dawa, vifaa tiba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameiagiza Kampuni tanzu ya Bohari ya Dawa (MSD) ya MSD- Medipharm Manufacturing Co.Ltd, kuzalisha dawa na vifaa tiba, ili kupunguza gharama za kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi, hasa bidhaa ambazo hazizalishwi na sekta ya binafsi.

Aidha, ameagiza MSD kutoa kipaumbele cha kununua dawa na vifaa tiba kutoka viwanda vya ndani, ili kupunguza gharama za kuagiza dawa nje ya nchi.

Ummy, alitoa agizo hilo jana Jijini Arusha, wakati akizindua kampuni tanzu pamoja na bodi yake, ambayo itaongozwa kwa muda na Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai.

"Kwa sasa asilimia 90 ya dawa na vifaa tiba, vinaagizwa kutoka nje ya nchi na wakati mwingine bidhaa hizo zinachukua miezi sita hadi mwaka kufika nchini na ndiyo sababu tumeona umuhimu wa kuanzisha kampuni hii ili kuongeza uzalisha wa dawa na vifaa tiba,"alisema.

Kwa mujibu wa Ummy, kampuni hiyo imeanzishwa ili kupunguza gharama za kuagiza dawa na vifaa tiba kutoka nje ya nchi itasimamia viwanda vyote vilivyopo chini ya MSD, huku akiiagiza kushirikiana na wabia kutoka sekta binafsi, ili kuzalisha kwa wingi zaidi na ubora unaotakiwa.

"Tumeianzisha kampuni hii, ili kuokoa fedha kigeni zinazotumika kuagiza dawa nje ya nchi kwa sababu bajeti yetu inatengwa kwa fedha za kitanzania kwa hiyo wakati wa kuzibadilisha kuwa fedha za kigeni gharama inaongezeka, lakini uwepo wa kampuni hii utasaidia kupunguza gharama hizo,"alisema.

Aidha, Ummy, alisema uwepo wa kampuni hiyo pia utasaidia viwanda vilivyo chini ya MSD kuongeza uzalishaji pamoja na kujenga viwanda vipya katika maeneo yanayomilikiwa na MSD ikiwemo Simiyu,Idofi mkoani Njombe,Zegereni -Pwani na Keko Dar es Salaam.

"Kwa sasa viwanda vilivyopo vikianza kufanya kazi kwa kasi pamoja na kuanzisha viwanda vipya itasaidia kuongeza ajira na kuimarisha utaalam wa ndani na katika mwaka huu mpya wa masomo ya elimu ya juu kupitia mfumo wa Samia tutatoka ufadhili kwa wanafunzi wanaosoma shahada ya pili ya "Industry Pharmacy,"alisema.

Mkurugenzi wa MSD Tukai, ambaye pia ni Mwenyekiti Bodi wa muda wa kampuni hiyo tanzu, alisema wanajivunia kuwa na kampuni hiyo ambayo itaongeza wigo wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba hapa nchini badala ya kuagiza nje ya nchi.

"Napenda kusema kwa miaka thelathini MSD ilikuwa inanunua,inatunza na kusambaza vifaa tiba lakini mwaka 2021 tulianza uzalishaji kwenye kiwanda chetu cha kutengeneza barakoa. Lakini kupitia kampuni yetu tanzu tuliyoizindua uzalishaji utaongezeka kwa kuwa itasimamia viwanda vyetu vyote na kuanzisha viwanda vipya,"alisema.

Alisema uwepo wa kampuni hiyo utasaidia kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 40 ambazo hutumika kila mwaka kuagiza dawa nje ya nchi kutokana na ongezeko la uhitaji wa dawa na vifaa tiba kutokana na serikali kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Mwenyekiti wa bodi ya MSD, Rosemary Silaa alisema wajumbe wa bodi ya kampuni hiyo ni watu wenye sifa na wabobezi kwenye sekta ya afya ambao watahakikisha kampuni hiyo inafanya vizuri kwa kusimamia viwanda vilivyokuwa vimeanzishwa na MSD.

# Mke mbaroni kwa kumwagia maji ya moto mumewe

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JESHI la Polisi mkoani Manyara, linamshikilia Flora Daniel, Mkazi wa Kazamoyo, Kata ya Endiamtu iliyoko Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya Simanjiro, kwa tuhuma ya kumwagia maji ya moto mume wake.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, George Katabazi, mtuhumiwa huyo alimwagia maji hayo yaliyoharibu mwili wa mumewe, Ouma Odauseri, Juni 18 mwaka huu.

Mtuhumiwa huyo, anadaiwa kutenda ukatili huo dhidi ya mumewe, kwa kumchoma kwa maji hayo mgongoni.

Alipotafutwa na Nipashe, kuzungumzia mkasa huo, Odauseri, alisema alifanyiwa siku hiyo, mke wake Flora Daniel, alimfuata na kuanza kumfokea na kisha kutumia maji ya moto aliyoyachemsha kwenye jiko la gesi kumwagia mgongoni.

Odauseri alisema chanzo cha kuunguzwa mgongoni na kumwagiwa maji ya moto na mke wake, ni ugomvi wa mara kwa mara, ambao unasababishwa na ukorofi wa mkewe.

Alisema ameishi na mke wake zaidi ya miaka 24, na wamejaliwa watoto watatu.

"Mke wangu, siku ya hilo tukio alikuwa ametoka kukesha disko na alirudi nyumbani kumekucha. Nikagombana naye, ndio akachemsha maji kwenye jiko la gesi na kunimwagia; ila kwa bahati nzuri, nikainama yakatua mgongono,"alisema Odauseri

Mwanaume huyo alisema miaka ya hivi karibuni wamekuwa na ugomvi wa mara kwa mara, lakini mwenza wake amekuwa akimpiga vibao na kumtukana kila wakati.

"Mke wangu ni mtu ambaye amezeeka, ila anaendekeza starehe kwa kulala disko na baa na anaweza kuondoka nyumbani hata mwaka na kurudi kibabe bila kutaka kuulizwa alipokuwa,"alieleza mume wa mtuhumiwa huyo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Kazamoyo, Hamad Mallya, alisema wamechoka kusuluhisha ugomvi wa wanandoa hao,na wanaona ni bora sheria ichukue mkondo wake.



Mdau wa Maendeleo, Mhandisi Manyango Nchimbi (kulia), akikabidhi msaada wa mahitaji mbalimbali muhimu ya watoto 100 wanaoishi mazingira magumu wa kata ya Nyamilangano na Iboja kwa msimamizi wao, Lucia Paul katika Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, mapema wiki hii. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanawake wapaza sauti vikwazo kugombea uongozi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAWAKE vinara wa uhamasishaji ushiriki wa wanawake katika masuala ya uongozi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, wameeleza changamoto wanayoiona tishio hivi sasa, ni wale walioshika madaraka hawana nia ya kuachia nafasi hizo.

Kutokana na ving'ang'anizi hao, wanawake wanaona ufinyu wa kupata nafasi nyingi za uongozi, kwa sababu viongozi wanaume wanataka kuongoza kwa muda mrefu.

Wakizungumzia nafasi ya mwanamke, wanawake hao vinara waliojengewa uwezo na Shirika la kiraia la TUSONGE CDO kutoka Wilaya za Siha na Moshi, mkoani Kilimanjaro, akiwamo Ruwaichi Shirima, Mkazi wa Kijiji cha Naibili, Kata ya Biriri, Wilaya ya Siha, alisema jambo kubwa zaidi ambalo hawatamani kuliona katika uchaguzi huo, ni matumizi ya rushwa.

"Kwa mfano, changamoto ninayoiona Biriri, ni kwamba wale wanaoshika madaraka hawataki kuachia nafasi wanazing'ang'ania; na kwa hiyo mwanamke anashindwa kupata nafasi, kwa sababu kiongozi mwanaume anaongoza kwa muda mrefu,"alisema.

Aidha, Neema Mwakaje, Mkazi wa Kijiji cha Korini Kusini, Kata ya Mbokomu, Wilaya ya Moshi, alisema picha anayoiona mbele kama wanawake wengi watapata nafasi za uongozi changamoto nyingi zinazowakabili zitapungua; na mfumo dume ambao unakandamiza wanawake wengi utakuwa unaondoka taratibu na kutakuwa na usawa.

"Maana tumeona katika jamii wanawake wengi hasa vijana wanakuwa na hofu ya kuingia katika uongozi. Hata katika kijiji chetu, wanawake wanahofu hiyo, wanadhani wakigombea hawatapata nafasi na wanawake wenzake wanaweza wasimchague.

"Nimezoea kuona wanaogombea na kuchaguliwa ni wa rika fulani, hasa wenye umri wa makamo na wazee, vijana wanakata tamaa ya kushiriki chaguzi nyingi kwa sababu ya jambo hilo."

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uliofanyika mwaka 2019, ni wanawake 4,171 tu, ndiyo walioshinda nafasi za wenyeviti wa vitongoji, sawa na asilimia 6.7, wanawake waliochaguliwa kuwa wenyeviti wa mitaa, walikuwa ni 528 kwa nchi nzima, sawa na asilimia 12.6; na wenyeviti wa vijiji, wanawake ni 246 tu, sawa na asilimia 2.1.

Mkazi wa Kijiji cha Kishisha, Kata ya Ivaeny, Wilaya ya Siha, Tumsifueli Kileo, alisema chanzo cha kuwa na idadi ndogo ya wanawake katika nafasi za uongozi, ni wanawake wengi kukosa elimu.

Alisema wanawake wengi wanapoitwa kwenye vikao, mikutano au vikundi hwataki kwenda, lakini laiti wangekuwa wanaenda, wangepata elimu na kujitokeza kugombea nafasi nyingi za uongozi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, akieleza mtizamo wa kiharakati kuhusu uchaguzi huo, alisema taasisi yao inaona uchaguzi huo unakwenda katika hatua ambayo kidogo, sasa umegusa yale mahitaji ya wana jamii.

"Ninaguswa kuona kwamba sasa hivi tunayo Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania (INEC), lakini suala la utekelezaji wa hilo, ni jambo jingine, kwamba inajiendesha kwa uhuru, au bado inajiendesha kwa kuangalia maslahi ya upande mmoja.

"Tuliloliona hasa ile mifumo ya vyama vya siasa, kuna kuwa na mambo mengi yanayorudisha nyuma akina mama kuingia katika mchakato wa uchaguzi na kuweza kufanikiwa. Moja, ile mfumo au taratibu za vyama vya siasa unakuta kuna vigezo; ni kama kwa makusudi vinaondoa akina mama nje.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# AMA WA LEO MMEMISI MENGI!

## -Wangapi wanakumbuka walivyoagana jioni kwa salamu za ndege yangeyange?

Na Adam Fungamwango

YANGEYANGE nipe kucha nyeupe, yangeyange nipe kucha nyeupe...” Ni wimbo maarufu wa zamani uliokuwa unaimbwa na watoto. Ndiyo, nasema watoto kwa sababu mtu mzima huwezi kumsikia akiimba wimbo huu, labda awe na matatizo ya akili.

Miaka hiyo kuanzia 1970, kuendelea hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 ulikuwa maarufu sana.

Tena nikuambieni tu vijana wa sasa ambao hamuufahamu wimbo huu, ulikuwa unaimbwa wakati maalum tu.Uliimbwa na watoto kuanzia miaka miwili mitatu hivi hadi 10, mpaka 12 hivi kutegemea na kukomaa kwa akili zao.

Uliimbwa jioni kuanzia saa 12:00 hivi jua likianza kuiangazia dunia upande mmoja.

Saa moja usiku ulikuwa ni mwisho wa kuimba wimbo huu. Kwa sababu giza lilikuwa limeingia.

Uliimbwa na kundi la watoto wanaojikusanya pamoja, wakirukaruka wakirusharusha mikono yao juu na kuishusha chini.

Wimbo huu haukuimbwa tu hivi hivi. Ni lazima kwanza angani kuwe na kundi la ndege wengi wenye rangi nyeupe ambao wanakuwa wanapita kurejea kwenye viota vyao kwenye kujipumzisha baada ya kazi kubwa ya kwenda kusaka chakula.

Ndege hao ambao hupenda sana kuishi maeneo ya pwani, au mwambao, huonekana asubuhi makundi kwa makundi angani wakienda kujitafutia chochote, na jioni kurejea kuashiria siku hiyo imekamilika kwao.

Asubuhi watoto wala hawajishughulishi kwa sababu wanadamka kwenda shule, ikifika jioni wanakuwa wameshapata chakula cha mchana, na mida hiyo wengi wao wanakuwa wamejikusanya na kucheza, kufurahia utoto wao.

Ndiyo muda kundi hilo la ndege kupita angani. Ni ndege ambao wana bahati kubwa ya kupendwa na watoto, kwani wakiwaona tu, wataacha kila kitu wanachokifanya na kuanza kuwafurahia jinsi walivyojipanga angani makundi kwa makundi, akipita kwa mbwembwe kama parade ya harusi au timu iliyotwaa ubingwa.

Watoto wanawasindikiza kwa wimbo huo nilioanza nao hapo juu hadi pale wanatapokuwa hawaonekani tena kwenye mboni za macho yao. Likipita kundi jingine hali inakuwa ni hiyo hiyo hadi giza linapoingia.

Sijajua asili ya wimbo huu, nani aliutunga, aliyeuanzisha na hata madhumuni yake.

Lakini kwa ajili ya utotoni enzi hizo iliaminika kuwa yeyote anayeimba na kurusharusha mikono yake wakati ndege hao wanapita, basi kucha zake zitakuwa nyeupe, kama rangi ya manyoya yao. Na kwa uthibitisho watoto wanaonyeshana kabisa kucha, kila mmoja anadai za kwake zimeshakuwa nyeupe zaidi kuliko kabla.

Hii ni moja kati ya dhana za watoto wa enzi hizo, ambao kwa sasa nao wameshakuwa watu wazima.

Na wakisoma hapa nadhani watakuwa wamenielewa, wengine wakitabasamu, wapo watakaocheka na wengine kukumbuka mbali sana enzi ya utoto wao.

Siwezi kumaliza makala haya, bila kumuelezea ni ndege wa aina gani, kwani wakati huo hakuna hata mtoto aliyejishughulisha kufahamu hilo.

Nadhani mpaka sasa ambao waliimba sana nyimbo hizo walikuwa wanawaona tu wakipita angani, lakini hawafahamu kiundani.



Picha zote zinawaonyesha ndege aina ya Yangeyange katika hali tofauti tofauti





**Yangeyange ni ndege wa aina gani?**

Ni jamii ya ndege wakubwa wenye miguu mirefu, shingo ndefu, midomo mirefu na myembamba.

Hapa utaona kuwa kumbe zamani tulikuwa tunawaona ni wadogo sana, kumbe kwa sababu wanapita wakiwa wameruka juu sana tena wakiwa kundi kubwa.

Hupinda shingo yao wakiruka angani. Rangi yao ni nyeupe ambao ndiyo kwa asilimia kubwa wapo hapa nchini na kuonekana kwa urahisi, lakini wapo wachache weusi, wanakula vyakula tofauti kutokana na upatikanaji wake.

Wengine hupenda kula samaki, baadhi hula wadudu na wanyama wadogo kama vyura, mijusi na panya.

Hujenga viota vyao juu ya matawi ya miti mbalimbali, ikiwemo mitete, ambako ndiyo hufanya kazi yao.

Hawa ndiyo yangeyange, ndege vipenzi vya watoto wa enzi hizo, ambao huwaimbia nyimbo nzuri, wakiamini kuwa ni ndege wazuri wenye roho njema na huweza kuwapa kile ambacho wanahitaji.

Ndiyo ndege pekee ambao walikuwa wakipita angani kwa mbwembwe na maringo, wanasindikizwa na nyimbo murua ambazo zinahanikiza na kuwasindiza safari ya kurudi makwao kwa usalama, wakipewa baraka tele na watoto hao ambao huachwa na furaha tele.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Putin aionya Korea Kusini kuwa itajuta kama....

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS Vladimir Putin, wa Russia, ameionya Korea Kusini kuwa itapata kile kinachostahili endapo itaipa Ukraine silaha.

Amesema itakuwa imefanya kosa kubwa, kauli ya kiongozi huyo inakuja baada ya serikali ya Korea Kusini kuweka wazi nia yake ya kupatia silaha Ukraine kama kujibu makubaliano mapya kati ya Russia na Korea Kaskazini.

Nchi hizo mbili hivi karibuni zilitiliana saini kusaidiana kijeshi iwapo kuna nchi moja imechokozwa na taifa lingine.

Rais Putin, alisema hawawezi kufurahishwa na uongozi wa sasa wa Korea Kusini na ikiwa itaamua kusambaza silaha kwa nchi ya Ukraine watajibu katika hali isiyopendeza.

Kiongozi huyo wa Russia alikuwa akizungumza nchini Vietnam, muda mfupi baada ya kumaliza ziara ya kiserikali nchini Korea Kaskazini.

Awali serikali ya Korea Kusini ililaani makubaliano hayo na kueleza ni tishio kwa usalama wa taifa lake.

Mshauri wa usalama wa taifa hilo, Chang Ho-jin alisema nchi yake inapanga kutafakari upya kuhusu suala la kupeleka msaada wa silaha nchini Ukraine.

Kufuatia matamshi hayo ya Rais Putin, ofisi ya rais wa Korea Kusini ilisema kwamba itaangalia machaguo mbalimbali katika kusambaza silaha kwa Ukraine na msimamo wake utategemea jinsi Russia inavyoshughulikia suala hilo.

Wakati huo huo, Korea Kusini imemwita balozi wa Russia kupinga mkataba wa ushirikiano wa kijeshi kati ya nchi yake na Korea Kaskazini.

Balozi Georgy Zinoviev anayeiwakilisha Russia nchini humo, aliitwa na serikali ya Korea Kusini kwa ajili ya kutoa maelezo ikiwa ni sehemu ya hatua ya kupinga makubaliano hayo.

Korea Kusini imeitaka Russia kuacha mara moja ushirikiano wa kijeshi na Korea Kaskazini na kuheshimu maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Korea Kaskazini imekuwa chini ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa tangu mwaka 2006 kutokana na mpango wake wa nyuklia uliopigwa marufuku.

Hapo awali hatua hizo ziliungwa mkono na Russia, lakini Rais Putin, alisema vikwazo hivyo vinapaswa kupitiwa upya.

Korea Kusini imetoa msaada wa kibinadamu na zana za kijeshi kwa Ukraine, lakini imekataa kutoa silaha hatari kwa vile ina sera rasmi ya kutozipa nchi silaha vitani.

Baadhi ya watu nchini Ukraine wamekuwa wakitumai kuwa ushirikiano wa kijeshi kati ya Russia na Korea Kaskazini ungeifanya Korea Kusini kufikiria upya mtazamo wake.

**BBC**



Vikosi vya usalama nchini Kenya vikikabiliana na waandamanaji jijini Nairobi juzi. **PICHA: REUTERS**

# Polisi yaua wakivunja maandamano Kenya

**NAIROBI**, KENYA

MTU mmoja ameuawa kwa kupigwa risasi na wengine kadhaa wametiwa mbaroni nchini Kenya katika maandamano ya kupinga muswada mpya wa fedha mwa mwaka wa 2024.

Kwa mujibu wa shirika la kimataifa la kutetea haki za binadamu la Amnest International, mtu huyo alipigwa risasi na polisi waliokuwa wakivunja maandamano hayo. Maandamano hayo sehemu kubwa yakihusisha vijana, yalianza katika jiji la Nairobi juzi kabla ya kusambaa katika miji mingine.

Waandamanaji walipinga mapendekezo ya serikali ya Rais William Ruto ya kuongeza ushuru katika bidhaa mbalimbali kupitia muswada huo wa fedha.

Vijana hao walisema wamechoshwa na sera za Rais Ruto, kuhusu uchumi katika kipindi ambacho idadi kubwa ya raia wa taifa hilo wanakabiliwa na ugumu wa maisha.

Licha ya maandamano hayo kuendeshwa katika hali ya utulivu, polisi waliwarushia waandamanaji mabomu ya machozi na maji ya kuwasha wakijaribu kuwazuia kuyafikia majengo ya bunge.

Kwa mujibu wa mamlaka huru ya kuangalia utendakazi wa polisi nchini humo, (IPOA), walipokea taarifa ya kufariki kwa mwandamanaji huyo na wameanzisha uchunguzi. Taarifa ya polisi ilisema mwanaume huyo mwenye umri wa miaka 29 alifariki baada ya kufikishwa katika hospitali moja jijini Nairobi akiwa na majeraha, lakini haikutoa maelezo zaidi.

Msemaji wa Amnesty International nchini Kenya, Mathias Kinyoda, alisema mtu huyo alipigwa risasi wakati akijaribu kuwakimbia polisi waliokuwa wakipambana na waandamanaji.

Aidha alieleza kwamba, mwanaume huyo alipigwa risasi na polisi mmoja ambaye hakuwa amevalia sare rasmi za kazi na kutaka uchunguzi ufanyike kuhusu tukio hilo.

**RFI**

# Wanajeshi 100 wauawa kambini Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

Burkina Faso imekabiliwa na shambulio zito katika kambi yake ya kijeshi na kusababisha kuuawa kwa wanajeshi zaidi ya 100.

Shambulizi hilo limesababisha kuwepo kwa uvumi wa mapinduzi kutokana na machafuko ndani ya vikosi vya usalama vya nchi hiyo.

Taifa hilo la Afrika Magaharibi limekuwa likiongozwa na serikali ya kijeshi tangu 2022.

Kiongozi wa kijeshi alionekana kwenye runinga ya serikali kukanusha uvumi huo wa uwepo wa mapinduzi mengine.

Burkina Faso imekuwa ikipambana na waasi wa Kiislamu kwa miaka kadhaa na takriban nusu ya nchi hiyo iko nje ya udhibiti wa serikali.

Kundi la jihadi la Jamaat Nusrat al-Islam wal-Muslimin (JNIM) lilisema limehusika na shambulio hilo lilotokea Jumanne iliyopita katika mji wa kaskazini wa Mansila.

Siku iliyofuata, kulitokea mlipuko karibu na makao makuu ya televisheni ya serikali.

Kulingana na ripoti kadhaa, watu wenye silaha Juni 11 watu wasiojulikana walishambulia kambi ya kijeshi, iliyoko karibu na mpaka na nchi ya Niger.

Ripoti zilisema wanajeshi 100 waliuawa na wengine wengi wametoweka.

Aidha, katika tukio hilo mamia ya raia walikimbia mji huo na kuelekea sehemu za jirani kutafuta usalama.

**BBC**

# Armenia yalitambua taifa huru Palestina

**YEREVAN,** ARMENIA

Wizara ya Mambo ya Nje ya Armenia, imetangaza kulitambua rasmi taifa huru la Palestina.

Pamoja na hatua hiyo, Armenia imesisitiza kuwa inaunga mkono azimio la Umoja wa Mataifa la kusitisha mara moja mapigano katika Ukanda wa Gaza, pamoja na suluhisho la mataifa mawili katika mzozo wa Palestina na Israel.

Hayo yanajiri wakati mapigano yakiendelea kuripotiwa huko Ukanda wa Gaza ambapo vikosi vya Israel vimeushambulia mji wa Rafah na maeneo mengine.

# MATUKIO KATIKA PICHA




Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Waumini wa Dini ya Kiislam, baada ya Ibada ya Sala ya Ijumaa katika Masjid Mushawar Mwembeshauri, Wilaya ya Mjini Unguja, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



Mabaki ya gari aina ya Toyota Noah yenye namba za usajili T 674 CSY iliyopata ajali na kuua watu wanne na kujeruhi wanne, katika kijiji cha Nkwae, kata ya Msisi, wilayani Singida mapema wiki hii. P**ICHA: THOBIAS MWANAKATWE**



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, SACP Augustino Senga, akizungumza wakati akitoa elimu ya Polisi Jamii kwa wakazi wa Kata ya Igamba, wilayani Mbozi jana. **PICHA: ISSA MWADANGALA**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akisalimiana na Mjumbe wa Kamati Kuu wa Chama cha Kikomunisti cha China na Katibu wa Kamati ya CPC Jimbo la Shanxi Tang Dengjie, kabla ya mazungumzo yao, katika Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu Magogoni, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**



Wafanya usafi wakifagia kuondo mchanga kwenye Barabara ya Malamba Mawili, eneo la Msigani Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-18

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

Majuzi alikuja mtu mmoja mlikuwa mnaongelea hili suala, lakini inaonekana kabisa hakukuwa na usahihi katika uchunguzi wa madaktari."

"Mimi mwenyewe nilikuja najiambia, kama nitabahatika kukutana na mchumba wa msichana yule ningemweleza ukweli wa hili suala. Mimi nafanya kazi kwenye ile hospitali. Niliwekwa kwenye uchunguzi wa pili, baada ya ule ya kwanza kutiliwa shaka."

"Enhee daktari, kwanza nataka uniambie, ule wa kwanza na wa pili upi ulikuwa sahihi?" "Wa pili!"

"Kwa nini?" Wa kwanza ulikuwa na shinikizo kutoka kwa watu fulani wenye uwezo. Walikuja wakamwaga pesa kwa baadhi ya madaktari wenzetu ili wapindishe uchunguzi. Na hao ndiyo walikuja kusema alianguka kwa kupatwa na presha ghafla barabarani akiwa anakimbia jogging alfajiri. Kelele zilivyopigwa na watu, pamoja na ndugu wa marehemu, kulikuwa na shinikizo kubwa, ikabidi madaktari wengine wateuliwe, siyo wale sasa. Ni sisi ambao tulikuja kugundua kuwa marehemu aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani. Wala hakuanguka kwa shinikizo la moyo." "Sasa umejuaje kama mimi siyo muuaji, wakati uchunguzi wa pili ulionyesha ameuawa?" Akaendelea kuuliza Kamal.

"Sisi wenyewe madaktari baada ya uchunguzi wa pili tukaanza kuulizana, ilikuwaje ikawa hivyo? Ndiyo tukapata taarifa za uhakika kuwa waliomuua ndiyo waliotumia pesa ili kupindisha uchunguzi wa kwanza. Na hao hao walitaka kushinikiza uchunguzi wa pili uwe kama wa kwanza, tukakataa. Tukautoa kama ilivyo. Tukapata taarifa sasa kuwa wale wale jamaa, wamekwenda kutoa pesa kwa baadhi ya askari polisi wasio waaminifu wamsingizie mtu kesi ya mauaji baada ya taarifa sahihi kutoka na kuwaridhisha ndugu na wananchi. Nilishangaa na kupatwa na simanzi niliposikia eti 'aliyepewa kesi ya kichwa', ni mchumba wake." Alisema dokta Shija huku akimtazama kwa masikitiko. "Pole sana kijana." Akamalizia.

Kamal akainua kichwa na kumtazama usoni daktari, akamjibu,"ahsante, ila kwa sasa haisaidii sana." Akahohoa kikohozi chepesi, halafu akamwambia,"ningeomba msaada wako." "Msaada gani kijana?"

"Kwa sababu upo mbele zaidi yangu kwa kulifahamu hili, unaweza kabisa kumshuku au kumfahamu muuaji."

"Kumfahamu siwezi kwa sababu sijamuona mtu yoyote ambaye amemuua mchumba wako, ila kuna kitu nitakusaidia ili angalau kumshuku tu, halafu mengine utajua mwenyewe." "Nitashukuru pia daktari."

"Ni hivi kijana, kwa sababu tayari kumeonekana kuna mkono wa mtu nyuma ya huu uchunguzi wa marehemu Mariamu, kitu kinachotakiwa mimi na wewe tujue, nyuma ya pazia kuna nani? Na tukimfahamu inawezekana kabisa kuwa tukatayemfahamu nyuma yake pia kuna mwingine." "Kwa nini unasema hivyo dokta?"

"Kijana kuua mtu ni jambo kubwa sana. Mtu anayetaka kufanya hivyo, au watu wanaotaka kuua kabla ya hayo wanakuwa na tahadhari kubwa sana. Wanaofanya hivyo bila kuchukua tahadhari wanakamatwa kirahisi sana.

Wale wanaoua kwa hasira au kukurupuka hawachukui muda, lakini hawa wanaonekana walikaa haswa wakapanga mauaji na wakachukua tahadhari zote kabla ya kutekeleza unyama wao." "Nadhani dokta pia wanatumia nguvu ya pesa kuficha maovu, kwa sababu wangekuwa wameshajulikana." "Kijana kuchukua tahadhari ya jambo lolote, binadamu anatumia rasilimali yoyote ile. Hawa ametumia muda, watu kama madaktari na mapolisi, pesa na vitu vingine kutekeleza na kuficha nyayo za ushahidi. Kwa maana hiyo hata hili unalosema lazima tuwe makini." "Mimi ninajua hilo, nimeshakuwa makini na ndiyo maana nipo hapa. Kulala hospitalini wakati siyo mgonjwa ni moja kati ya kitu ninachoamoni kimenisaidia kuwepo huru mpaka sasa. Vinginevyo ama ningekuwa nimekamatwa, au nimeuawa. Usidhani hapa natafutwa na polisi peke yake, hata hao wauaji wananisaka."

Ndipo dokta Shija alipomuangalia kwa makini Kamal na kutasamu kidogo akimsifu kimoyomoyo kwa ujasiri na ujanja alioufanya ili kujificha. Ana wiki kadhaa analala hospitalini hapo kwa kulipia kama mgonjwa, huku mwanzo alipofika alidai anaumwa, lakini walipompima hakuonekana na ugonjwa wowote.

"Sawa, nakuahidi nitakusaidia." Dokta akamuahidi.

Dokta Shija alijua anaweza kupata fununu kwa madaktari wenzake ambao walipewa rushwa na kubadilisha uchunguzi. Yoyote ambaye atatajwa, atakuwa ni mmoja kati ya watu walio kwenye mpango mahsusi wa kumuua marehemu Mariamu.




**Siku hiyo alipata makazi mapya. Ilikuwa maeneo ya kurasini kwenye mabehewa chakavu ya relwe. Alipata ruhusu ya kulala hapo na walinzi wawili ambao waliwaambia alifika Dar kutoka Kigoma, lakini hakumkuta mwenyeji wake na alikuwa amezima simu.**

****************************************

Siku ile ile, Kamal alihama hospitalini hapo. Kama kawaida yake ya kutomuamini mtu yoyote, alitumia kanuni hiyo hiyo kukacha kulala hapo. "Kama madaktari wenzake walichukua mlungula na kubadilisha uchunguzi kuonekana ameanguka kwa presha kumbe ameuawa, kwa nini isiwezekane na yeye achukue pesa na kuwaambia wabaya wake au askari polisi kuwa yupo kwenye hospitali ile?" Akawaza.

Mwanzoni alilala hapo kwa sababu siri ile alikuwa anaijua yeye mwenyewe. Hakuna aliyejua kuwa mtuhumiwa na mauaji ya Mariamu ambaye ni mchumba wake yupo pale.

Siku hiyo alipata makazi mapya. Ilikuwa maeneo ya kurasini kwenye mabehewa chakavu ya relwe. Alipata ruhusu ya kulala hapo na walinzi wawili ambao waliwaambia alifika Dar kutoka Kigoma, lakini hakumkuta mwenyeji wake na alikuwa amezima simu.

Akawaambia kuwa hakuwa na chochote kile, chakula wala sehemu ya kulala. "Nilikuwa nawasiliana naye wakati nakuja Dar na yeye ndiye aliyeniambia nije, nashangaa kufika hapa kanizimia simu na hapatikani tena."

Walivyomuona, na jinsi alivyovaa, waliamini na kuamua kumkaribisha. Wakampa chakula na kumpa ruhusa ya kulala ndani ya moja ya mabehewa chakavu. Waliamini ndugu yake huyo anaweza kupatikana hewani baada ya siku chake, kwani huenda aliporwa na vibaka wakati anawasiliana naye.

Alichofanya Kamal, ni kutoka na kibegi chake kwenye hospitali aliyokuwa kama amekodi ambaye alilala kwa siku kadhaa, akaenda kuoga na kubadilisha nguo zake katika bafu moja pale, Ilala Karume nje ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), akavaa nguo zilizomfanya awe na muonekana kama mtu aliyechoka hivi, fukara, masikini, hana kitu, mchovu, ndipo alipokwenda maeneo ya Kurasini ambako, baadhi ya vichwa vya treni na mabehewa hufanyiwa matengenezo.

Alichowaza ndicho kilichotokea, nia yake ilikuwa ni kulala kwenye mabehewa mabovu ambayo hayatumiki tena. Lakini ilikuwa na lazima kuwakabili walinzi kwa uongo. Akafanikiwa. Nia ilikuwa ni kutoendelea kuishi tena hospitalini kwa ajili ya usalama. Alitaka kuwasiliana na dokta Shija akiwa haishi tena hapo.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# PAMBA JIJI FC YAKANUSHA KUTIMUA WACHEZAJI WOTE

Na Faustine Feliciane

UONGOZI wa Pamba Jiji FC ya jijini Mwanza umesema si kweli wamefukuza wachezaji wake wote waliokuwa katika kikosi chao ambao walipambana na kuipandisha daraja timu hiyo ili kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, imeelezwa.

Pamba Jiji FC ilimaliza katika nafasi ya pili katika Ligi ya Championship msimu uliomalizika nyuma ya mabingwa, KenGold ya Mbeya ya kukata tiketi ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/2025.

Mwenyekiti wa Pamba Jiji, Bhikhu Kotecha, akizugumza na gazeti hili jana alisema wachezaji wengi wa timu hiyo wamemaliza mikataba yao baada ya kumalizika kwa msimu msimu uliopita na si kweli wamewaacha wote.

"Hatuwezi kuacha wachezaji wote, kilichotokea baada ya kumalizika kwa msimu wachezaji wengi wamemaliza mikataba yao, kama uongozi hatuwezi kuwaacha wachezaji wote, tutakaa na kufanya upembuzi na kuona nani na nani tuwaongezee mikataba na nani wa nje tumuongeze katika kikosi kuelekea msimu mpua.

Tunafahamu Ligi Kuu ni ngumu na lazima tujipange na kuwa na wachezaji bora ambao watatusaidia kufikia kwenye malengo katika ligi hiyo ambayo inaushindani na changamoto mbalimbali," alisema Kotecha.

Aliongeza taarifa zinasemwa sasa si nzuri kwa sababu zinawaweka katika nafasi ya kuonekana ‚wamewatupa' nyota ambao walijituma na kuirejesha heshima ya Pamba Jiji iliyoshuka daraja mwaka 2001 na msimu ujao itakuwa chini ya Kocha Mserbia, Goran Kopunovic.

"Maneno yanasemwa na watu wasioitakia mema klabu yetu hasa baada ya kuiona imefanikiwa kupanda daraja. Mbona hizi kelele tulikuwa hatuzisikii kabla ya timu kupanda, hawa ni watu wasiotutakia mema katika safari yetu mpya, Wana-Mwanza watulie na kila kinachoendelea watafahamishwa tu," alisema Kotecha.

Mwenyekiti huyo pia aliishukuru Serikali ya Mwanza chini ya Mkuu wa Mkoa kwa namna wanavyoshirikiana na kuwaunga mkono wakati wote.

Alisema pia klabu itaendelea na mikakati kwa ajili ya kuhakikisha wanasajili kikosi imara na wamepanga kuanza mapema maandalizi ya msimu mpya.

"Tumerejea katika Ligi Kuu, tunataka tuwe moja ya timu zinazoshindana kweli kweli, tunataka kuanza vyema msimu mpya, hii ndio ndoto ya wakazi wa Mwanza ambayo waliisubiri kwa muda mrefu," Kotecha aliongeza.



Mchezaji yosso wa Yanga (kulia), akipiga shuti huku akidhibitiwa na nyota wa KMC katika mechi ya Ligi ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (U-17) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ulioko Kigamboni, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 5-1. **PICHA: TFF**

# Waogeleaji chipukizi kuchuana Dar

Na Shufaa Lyimo

WAOGELEAJI 300 kutoka katika klabu 14 za Tanzania Bara na Zanzibar wanatarajia kushiriki mashindano ya vijana yatakayofanyika kuanzia leo na kesho kwenye bwawa la kuogelea Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST) jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa Habari wa Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Sebastian Kolowa, aliliambia gazeti hili mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji wenye umri chini ya miaka 11.

„Lengo la mashindano hayo ni kuunda Timu ya Taifa ambayo itashiriki mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, tunaomba wadau wajitokeze kuona vipaji vya vijana wetu kuanzia kesho (leo)," alisema Kolowa.

Mratibu huyo alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vyema na wanatarajia kuona upinzani mkubwa kutokana na idadi kubwa ya washiriki waliothibitisha kushindana.

Aliongeza waogeleaji kutoka nje ya Dar es Salaam wameshawasili kuanzia juzi na waliendelea na mazoezi ili kuimarisha viwango vyao.

„Ninawaomba mashabiki na hasa vijana kutoka kila mahali wajitokeze kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa na waogeleaji kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, tunaamini tutakuwa na mashindano yenye upinzani na yatatusaidia kufikia malengo ya kuteua timu ya taifa," Kolowa alisema.

Aliongeza TSA inafutahi kuona mchezo huo kwa sasa unaendelea kukua kwa sababu idadi kubwa ya Watanzania wameanza kuufahamu tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma ambapo waliamini ni mchezo wa hatari na unawahusu familia zenye uwezo mkubwa kifedha.

# Katambi mwenyekiti mpya mpira wanawake Shinyanga

Na Somoe Ng'itu

HAMISA Katambi amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Shinyanga (SHIWFA), katika uchaguzi uliofanyika kwenye Ukumbi wa Uwanja wa Kambarage mkoani humo juzi.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kutangaza mshindi wa nafasi hiyo, Katambi alisema anataka kuona soka la wanawake Shinyanga linachezwa kuanzia ngazi ya kati, wilaya na mkoa.

Mwenyekiti huyo alisema anaamini kwa kufanya hivyo, wataibua vipaji na hatimaye Shinyanga kupata timu itakayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

„Nawashukuru wajumbe wa kunipa heshima ya kuwa Mwenyekiti wa SHIWFA, ninawaahidi sitawaangusha, tutajipanga na kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuifanya Shinyanga yetu iwe juu jkatika soka la wanawake, ndoto zetu ni kupata timu itakayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake," alisema Katambi.

Nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA ilichukuliwa na Tabia Chepe huku Justina Venant na Elizabeth Njile walichaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya SHIWFA.

Wakati huo huo, Chama cha Soka cha Wanawake Mkoa wa Tabora kilifanya uchaguzi wake juzi na Farida Ndyamkama, amechaguliwa kuwa mwenyekiti wa chama hicho akimshinda Leticia Bundala.

Nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa ikienda kwa Anna Mwingira na Tausi Changuluma alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji.

Tayari mikoa 20 ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Simiyu, Katavi, Kigoma, Kagera, Tanga, Arusha, Mtwara, Rukwa, Manyara na Singida imefanya uchaguzi kwa ajili ya kujiandaa na mchakato wa uchaguzi wa TWFA utakaofanyika baadaye mwaka huu.

TWFA ni mwanachama shirikishi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambayo pia itafanya uchaguzi wake mkuu hapo mwakani baada ya viongozi waliopo kumaliza muda wao wa kikatiba wa miaka minne.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

### GULER ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL inamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uturuki mwenye umri wa miaka 19, Arda Guler, kutoka Real Madrid. (***Teamtalk***)

### CHALOBAH ATAJWA FULHAM

KLABU ya Fulham inayoshiriki Ligi Kuu England imefufua nia yao ya kumnunua beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24,Trevoh Chalobah. (***Standard***)

### UNITED YAMTOSA BRANTHWAITE

KLABU ya Manchester United itaachana na mazungumzo na Everton kwa ajili ya kumnunua mlinzi, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21, endapo The Toffees hawatapunguza bei ya pauni milioni 70. (***ESPN***)

### YORO AICHAGUA MADRID

MLINZI wa Lille, Leny Yoro, mwenye umri wa miaka 18, anapendelea kuhamia Real Madrid badala ya Liverpool au Manchester United . (***Marca***)

### KUDUS AJIPANGA KUONDOKA

WEST Ham inahofia winga wa Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 23, ataomba kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto. (***Football Insider***)

### SOULE ATAKIWA VILLA

ASTON Villa imeuliza kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Argentina, Matias Soule, mwenye umri wa miaka 21, lakini Juventus inasema hauzwi. (***Sky Sports***)

### ANSELMINO KUTUA CHELSEA

CHELSEA ipo katika mazungumzo na Boca Juniors kuhusu dili la kumnunua beki wa Timu ya Taifa ya Argentina mwenye umri wa miaka 19, Aaron Anselmino. (***Athletic***)

### ZIRKZEE AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United inajiandaa kutumia kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 33.8 katika mkataba wa mshambuliaji wa Bologna, Mholanzi Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 23. (***Telegraph***)

### BAYERN YAMTAKA SIMONS

KIUNGO wa kati wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Xavi Simons, mwenye umri wa miaka 21, ndiye anayelengwa na Bayern Munich ya Ujerumani. (***Bild*** )

### WAARABU WAMTAKA PIOLI

KOCHA wa zamani wa AC Milan, Stefano Pioli, ni miongoni mwa walimu wanaowania na Klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia. (***Fabrizio Romano***)

### KADIOGLU ATAJWA ARSENAL

ARSENAL imewasilisha ombi la kumnunua beki wa pembeni wa Fenerbahce ya Uturuki, Ferdi Kadioglu, mwenye umri wa miaka 24. (***Ajan Spor***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UEFA YAJIPANGA KUMZUIA MBAPPÉ

**MUNICH,** Ujerumani

**Ni katika kuvaa maski yenye rangi tatu za bendera ya...**

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappé, anatazamiwa kuzuiwa kuvaa maski ambayo ameionyesha juzi yenye rangi tatu za bendera ya nchi yake, atakaporejea uwanjani katika michuano ya Euro 2024.

Mbappé alivunjika pua katika ushindi wa bao 1-0 wa Ufaransa dhidi ya Austria Jumatatu iliyopita wakati uso wake ulipogongana na bega la mlinzi wa Austria, Kevin Danso.

Akiwa anatazamia kurejea haraka uwanjani, fowadi huyo wa Real Madrid alijiunga na mazoezi mepesi na wachezaji wenzake juzi huku amevalia maski ya tricolore ambayo ni maarufu huko Ufaransa.

Hata hivyo, sheria za Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), zinamaanisha Mbappé ataruhusiwa tu kuvaa maski yenye rangi moja.

**"Vifaa vya matibabu vina vyovaliwa uwanjani lazima viwe na rangi moja na vi sivyo na utambulisho wa timu na mtengenezaji," in asomeka sehemu ya kanuni za UEFA.**

Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps, alisema Alhamisi ana matumaini Mbappé anaweza kucheza haraka na hakuna uwezekano wa kucheza mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi pale Ufaransa itakapoikabili Poland Jumanne.

"Kila kitu kinakwenda sawa, baada ya mshtuko tuliokuwa nao. Aliweza kushiriki katika mazoezi mepesi juzi, na itakuwa hivyo. Kila kitu kinabadilika katika mwelekeo sahihi.

Tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha atapatikana haraka." alisema Deschamps.

## HABARI MICHEZO

# MESSI: USHINDI MECHI YA UFUNGUZI HULETA UTULIVU



**ATLANTA,** Marekani

LIONEL Messi amesisitiza umuhimu wa Argentina kuanza michuano ya Copa América kwa mguu wa kulia kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Canada hapo juzi kutawapa utulivu.

Messi, ambaye aliweka rekodi ya Copa América kwa kucheza mechi yake ya 35, alisema: „Ushindi huo unakupa utulivu kwa sababu unateseka sana unapoanza kwa kupoteza.

"Hatukuwa na uzoefu wa kuanza mashindano kwa ushindi kabla chini ya Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni."

Hata hivyo, mwanzo mbaya haujaiumiza Argentina katika miaka ya hivi karibuni.

Walitoka sare mechi ya kwanza ya Copa América 2021 na Chile lakini wakashinda mashindano hayo.

Katika fainali za Kombe la Dunia la 2022, walichapwa 2-1 na Saudi Arabia, na hivyo kumaliza mfululizo wa mechi 36 bila kushindwa, na bado wakaishinda Ufaransa kwenye fainali.

Argentina sasa wanatafuta taji lao kuu la tatu mfululizo na Messi alisema lazima waendelee kucheza kama timu.

"Tangu mwanzo, kundi hili lilithibitisha ni timu na hivyo ndivyo tulivyofanikisha kile ambacho tumefanikiwa," alisema fowadi huyo wa Inter Miami.

"Njia pekee ya kuifanikisha tena ni kuendelea kwa namna hii."

Messi, ambaye atatimiza umri wa miaka 37 Jumatatu ya Juni 24, alikuwa muhimu kwa mabao yote mawili ya Argentina dhidi ya Canada.

Mpira wake wa juu ulipelekea Julián Álvarez kufunga bao la kuongoza, kabla ya kutoa asisti kwa Lautaro Martínez aliyefunga bao la pili dakika ya 88.

"Tulijua itakuwa ngumu," alisema. „Tulitarajia mchezo mgumu sana na wa kimwili. Wakati mwingine tunapata ugumu wa kupata nafasi lakini tunahitaji kuendelea.

"Wengi wa wapinzani wetu wanacheza tofauti dhidi yetu, tunahitaji kudumisha udhibiti."

Argentina watarejea uwanjani Jumanne watakapomenyana dhidi ya Chile kwenye Uwanja wa MetLife huko New Jersey.

"Sasa tunapaswa kucheza dhidi ya timu ya taifa yenye ushindani mkubwa Chile, ambayo kwa kuwasili kwa kocha Ricard Gareca imepata faida zaidi," alisema Messi.

# Baggio, familia wavamiwa



**VICENZA,** Italia

NYOTA wa soka mstaafu wa Italia, Roberto Baggio, alivamiwa nyumbani kwake na watu wenye bunduki wakati alipokuwa akitazama mchezo wa timu ya taifa dhidi ya Hispania kwenye michuano ya Ulaya hapo juzi.

Majambazi watano wenye silaha walivamia nyumba ya kifahari ya Baggio iliyopo karibu na jiji la Kaskazini la Vicenza kati ya saa 10 jioni kwa saa za huko wakati akiwa ndani, kwa mujibu wa na ripoti za vyombo vya habari vya Italia.

Mmoja alimpiga Baggio kichwani na kitako cha bunduki wakati mchezaji wa zamani wa soka alipokabiliana nao.

Majambazi hao walimfungia Baggio mwenye umri wa miaka 57 na familia yake ndani ya chumba huku wakiiba vito, saa na fedha taslimu.

Baada ya wezi hao kuondoka, Baggio alivunja mlango na kuwaita polisi.

Alipelekwa hospitali na kushonwa nyuzi za jeraha. Watu wa familia yake hawakudhurika.

Baggio aliichezea Italia mechi 56, akifunga mabao 27.

Hispania ilishinda mechi dhidi ya Italia mjini Gelsenkirchen 1-0.

# Kocha Hispania atamba hakuna timu iliyowazidi

**GELSENKIRCHEN,** Ujerumani

LUIS de la Fuente amesema hakuna timu bora kuliko Hispania baada ya kuifunga Italia bao 1-0 katika mechi iliyochezwa juzi na kuifanya kupata ushindi wa pili pamoja na kukata tiketi ya kuingia hatua ya mtoano ya michuano ya Euro 2024.

Bao la kujifunga la kipindi cha pili kutoka kwa mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori, lilileta tofauti hiyo kwenye Uwanja wa Arena AufSchalke, lakini kocha wa Hispania, De la Fuente, alihisi bao hilo liliwanyamazisha Azzurri.

„Sio tu ushindi, ni jinsi tulivyofanya dhidi ya mabingwa wa sasa wa Ulaya," alisema De la Fuente wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

"Tulikuwa bora zaidi kimwili, kimbinu na katika masuala ya vipaji vya wachezaji wetu.

„Tuliitawala na kuidhibiti Italia na tungeshinda kwa zaidi kwa nafasi tulizopata. Kuna nafasi ya kuimarika, lakini tuliona uwezo ambao timu hii ya Hispania inao, ikibatilisha timu kama Italia. Sasa inabidi twende hatua kwa hatua."

Hispania walipiga mashuti 21 dhidi ya matatu ya Italia huku wakiwa timu ya pili kutinga hatua ya 16 bora baada ya wenyeji Ujerumani.



"Wakati raundi ya mtoano inapoanza inategemea mambo madogo," De la Fuente aliongeza alipoulizwa kama maendeleo ya mapema ya Hispania na Ujerumani yaliwafanya kuwa na nafasi kubwa kubeba taji hilo.

"Hakuna bora zaidi ya Hispania, lakini tunapaswa kuwa waangalifu, haitakuwa rahisi, timu zingine zitatujua zaidi, lakini bado nasema tukifanya kazi vizuri, hakuna timu bora kama sisi.

"Kwa maoni yangu, Hispania wana soka bora zaidi duniani. Lakini najua timu hii inaundwa na nini na sote tunajua bado hatujafanya chochote. Tunapaswa kuwa waangalifu, wanyenyekevu na heshima."

Hatima ya Italia katika dimba hilo itaamuliwa katika mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi dhidi ya Croatia hapo keshokutwa, ingawa bado wako katika nafasi nzuri ya kusonga mbele baada ya kuifunga Albania katika mechi yao ya kwanza.

Nico Williams alikuwa mkali hasa, huku winga huyo wa Athletic Club akisaidia kutengeneza bao la Hispania na kupata tuzo ya mchezaji bora wa mchezo.

## Nyota Taifa Stars awaita wadhamini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHEZAJI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Novatus Dismas (20), anayecheza katika Klabu ya Shakhtar Donetsk ya Ukraine, amefungua rasmi michuano ya East African Cup akimwomba, Rais Samia Suluhu Hassan, kuifadhili ili kuibua vipaji vya wachezaji chipukizi.

Novatus, ambaye kipaji chake kiliibuliwa kupitia mashindano hayo, alifungua michuano hiyo jana, inayoendelea kwenye Shule ya Ufundi Moshi.

Nyota huyo ameliomba pia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuitizama michuano hiyo na kuisapoti, kwa sababu vijana wengi wenye vipaji watapatikana na kuja kulisaidia taifa katika mashindano mbalimbali ikiwamo Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

"Ni ushauri na ombi pia kwa watu wanasiasa, na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwashika vijana mkono vijana ili waweze kufikia malengo yao.

Kuwa na mashindano mengi kama East African Cup, ni kitu kizuri ambacho kitawafanya vijana wapate fursa ya kuonekana na kupata nafasi katika sehemu mbalimbali," alisema Novatus.

Mratibu na mwandaaji wa michuano hiyo, Prisca Lema, alisema mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka mkoani Kilimanjaro, mwaka huu yameshirikisha timu 28.

"Tuna wachezaji wa umri chini ya miaka 13 na 16 kwa wasichana na wavulana. Kwa mwaka huu kuna mchezo mpya tutauanzisha ambao ni mpira wa kikapu.

East African Cup, imekuwa ni moja ya jukwaa kubwa ambalo linaibua vipaji kwa vijana wa kike na wa kiume lakini pia marefa na makocha ambao wanafanya vizuri sana nchini Tanzania," alisema mratibu huyo.

# KISINDA ATAJWA KUTAKIWA COASTAL UNION 2024/2025

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikianza kutangaza majina ya wachezaji inayowaacha, Coastal Union iko mbioni kumsajili winga wa zamani wa Yanga, Tuisila Kisinda, lengo ikiwa ni kujiimarisha kuelekea mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, imefahamika.

Habari kutoka ndani ya Coastal Union zinasema mazungumzo na Kisinda yameshaanza, na endapo yakienda vyema, basi mchezaji huyo atamwaga wino katika klabu hiyo.

"Tunaendelea na usajili, na tunalenga wachezaji ambao ni wazoefu kwenye michuano ya kimataifa, huwezi kwenda kucheza huku ukiwa na vijana wengi, wakongwe, siyo wa umri, ila kwenye mechi kubwa wanahitajika, hivyo tunamkata Kisinda, najua atakuja kutusaidia kwa sababu amecheza klabu kubwa kama AS Vita, Yanga na RS Berkane," kilisema chanzo chetu.

Siku chache kabla ya taarifa hizi, Ofisa Habari ya Klabu hiyo, Abbas El Sabri, alikiri kufanya mazungumzo ya mchezaji mwingine raia ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Djuma Shaaban.

"Ni kweli tupo katika mazungumzo na Djuma, ni mchezaji mzuri, mzoefu katika mechi za kimataifa. Unajua tangu tulipopata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho, tayari kama klabu tukatambua mahitaji yetu yataongezeka, kuanzia gharama, wachezaji na hata muda utakuwa finyu," alisema El Sabri.

Mbali na huyo ambaye Coastal Union imekiri, lakini taarifa zinasema wanaendelea na mazungumzo na Saido Ntibazonkiza kama ambayo gazeti hili liliripoti hivi karibuni kabla ya hata ya kuachwa na Simba.

Wakati huo huo, klabu hiyo imeanza kutoa majina ya wachezaji inayoachana nayo, ambapo imewatangaza, Roland Beako na Aboubakar Abbas, hawatakuwa sehemu ya kikosi chao katika msimu mpya.

Kisinda amezichezea Yanga na RS Berkane ya Morocco kwa vipindi viwili tofauti kwa kila timu, akisajiliwa kutoka AS Vita mwaka 2021, akaenda RS Berkane mwaka 2022, lakini alirejeshwa kwa mkopo na mwaka jana alirejea kwenye klabu yake ya awali na sasa amemaliza mkataba.



Waamuzi waliochezesha mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Wanawake Daraja la Kwanza kati ya Ruangwa Queens ya Lindi dhidi ya Sayari Womens kutoka Dar es Salaam wakitakiana heri kabla ya kuanza kwa mechi hiyo kwenye Uwanja wa Fountain Gate jijini, Dodoma jana. **PICHA: TFF**

## Simba SC, Coastal zamgombea Lawi

INATOKA UK. 24

Aliongeza bado hawajamaliza kutangaza wachezaji wanowaacha kwa sababu wanataka kuongeza 'majembe' yatakayokuja kuendeleza mazuri ndani ya kikosi chao.

"Tulisimama kuendelea kutangaza nyota tunaowaacha kwa sababu tulitaka kuwabadilishia ladha mashabiki kwa kumtangaza mchezaji wa kwanza tuliyemsajili, sasa tunarejea tena kuwatangaza tunaowaaga," alisema Ahmed.

Naye Msemaji wa Coastal Union, Abbas El Sabri, aliiambia gazeti hili, Lawi bado ni mchezaji wa Coastal Union baada ya Simba kutofuata taratibu walizopeana katika kumsajili beki huyo.

"Huo usajili tunausikia tu katika mitandao, Lawi ni mchezaji wetu, ni kweli Simba walileta ofa na sisi tukawapa utaratibu wetu kukamilisha usajili huo, lakini sijui walikutwa na nini hawakufuata huo utaratibu, tulipoona wenzetu wanachelewa tukakaa na mchezaji na kumweleza mipango yetu na kuamua kubaki naye kikosini, Lawi bado mchezaji wetu," alisisitiza El Sabri.

# Yanga yaanika rasmi malengo matatu CAF

INATOKA UK. 24

tuvunje rekodi yetu wenyewe, tukifika nusu fainali tu tutakuwa tayari tumeshafanya hivyo.

Chochote kikitokea baada ya hapo ni mafanikio, lakini bado ikitokea tukienda fainali ni moja ya malengo tuliyojiwekea na kuchukua ubingwa pia ikiwezekana, hilo kwetu linawezekana kutokana na kikosi tutakachokijenga msimu ujao," Kamwe alisema. Wakati huo huo, Mabosi wa Yanga wamesema wamemwongeza mkataba wa mwaka mmoja kiungo mkabaji, Zawadi Mauya.

Kamwe alisema Mauya ataendelea kusalia ndani ya kikosi hicho kutokana na mchango wake bado unahitajika.

Hata hivyo taarifa kutoka Yanga zinasema Mauya amepewa mkataba mpya kutokana na klabu hiyo kumkosa, Yusuph Kagoma aliyekuwa anaitumikia Singida Black Stars, kudaiwa tayari ameshamalizana na watani zao, Simba.

Chanzo chetu kinasemea klabu hiyo pia inajipanga kuwaongeza mikataba wachezaji wake, Salum Aboubakar 'Sure Boy', Jonas Mkude, Kibwana Shomari na nahodha, Bakari Mwamnyeto ili waendelee kukipiga katika kikosi hicho kilichotwaa ubingwa wa Tanzania Bara mara 30.

"Yanga haitaki kupoteza wachezaji wengi ambao iliwasaidia kufika ilipofika, itawabakisha wale nyota, halafu inatarajia kuwapa mikataba wale ambao walikuwa hata hawachezi mechi nyingi kwa sababu imeonekana hata wakiingia wanatekeleza kile ambacho mwalimu anakitaka, mfano mechi dhidi ya Mamelodi Sundowns ilipowakosa wachezaji wake nyota," kiliongeza chanzo chetu.

Yanga itatajwa pia iko mbioni kukamilisha mazungumzo ya kumnasa beki wa kushoto wa FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Chadrack Boka, ili kuchukua nafasi itakayoachwa na Joyce Lomalisa, aliyemaliza mkataba wake huku Mkongomani mwingine, Emmanuel Lobota, anayecheza nafasi ya winga, kutoka Singida Black Stars na Agee Basiala, kiungo wa DR Congo, anayekipiga kwenye Maniema Union huenda wakatua Jangwani.

Michezo
Jumamosi Juni 22, 2024
Nipashe



UEFA yajipanga kumzuia Mbappé
UKURASA 21



Nahodha wa Hispania, Alvaro Morata (katikati), akiwa anapambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Italia katika mechi ya Kundi B ya michuano ya Euro 2024 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Arena AufSchalke jijini Gelsenkirchen, Ujerumani juzi usiku. Hispania ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yaanika rasmi malengo matatu CAF

## ●●● Yatamba kubeba ubingwa Afrika inawezekana, yampa Mauya mkataba...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamesema malengo yao kuelekea msimu mpya wa mashindano wa mwaka 2024/2025 ni kufika hatua ya nusu fainali, fainali au kubeba taji la Afrika, imeelezwa.

**Msimu uliopita Yanga ilitolewa katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jeuri ya kuzungumza matarajio hayo wanaipata kutokana na kikosi kilichopo, na kile ambacho watakiongeza kuelekea msimu ujao.

Kamwe alisema wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kubakisha wachezaji tegemeo, hivyo kikosi kitakuwa na makali zaidi kwa sababu kitaundwa na nyota wale wale lakini watakiboresha kwa kuongeza wengine ambao wana viwango vikubwa zaidi na kuifanya timu hiyo kuwa tishio.

"Kwanza tumefanikiwa kumbakisha Kocha Miguel Gamondi, hiyo peke yake ni jambo kubwa sana, lakini tumewabakisha wachezaji wetu tegemeo ambao walituheshimisha msimu uliopita, kama vile haitoshi tunaongeza na mashine nyingine.

Nimechungulia mimi majina ya wachezaji wapya, ni hatari, yaani msimu ujao mbali na kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA, tuna malengo mengine matatu, kwanza kabisa ni akili yetu ni kutwaa ubingwa wa Afrika, kama tukishindwa basi tufike fainali tu, na kama ikishindikana tuishie nusu fainali," alisema Kamwe.

Aliongeza hatua hizo tatu itakuwa ni heshima kubwa kwa Yanga kwa sababu haijawahi kufikia hatua hiyo tangu mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yalipoanzishwa.

"Tulikuwa hatujaingia hatua ya makundi kwa miaka 24 hivi, tukaingia na msimu huo huo tukafika robo fainali ambayo tulikuwa hatujawahi kufika tangu mfumo huu wa makundi uanze, na huu ulikuwa msimu mmoja tu, sasa msimu wa pili tunahitaji

INAENDELEA UK. 23

## Simba SC, Coastal zamgombea Lawi

**Faustine Feliciane na Somoe Ng'itu**

WAKATI Simba ikitangaza itaenda kuweka kambi yake katika jiji la Ismailia, Misri, mabosi wa klabu hiyo wamesema walifuata taratibu zote katika mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Coastal Union, Lameck Lawi, imefahamika.

Uongozi wa Coastal Union umesema Lawi bado ni mchezaji wao halali na wanashangaa kuona Simba imemtangaza beki huyo kuwa ni mali yake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Crescentius Magori, alisema klabu hiyo ililipa awamu ya kwanza ya fedha kwa Coastal Union na kiasi kilichosalia walitakiwa kukikamilisha Mei 31, mwaka huu.

Magori alisema Coastal Union ilipaswa kuandika barua ndani ya siku 10 endapo Simba ilichelewa kukamilisha malipo lakini haikufanya hivyo.

Kiongozi huyo alisema Simba ilifuata taratibu zote na ilikamilisha malipo ya awamu ya pili ndani ya muda.

"Huu mpira ni wa FIFA, haushii Karume (ilipo Shirikisho la Soka Tanzania- TFF), hawa wameingia tamaa baada ya mchezaji kupata timu nje, sasa wamuuze, tutawashitaki Coastal pamoja na timu itakayomnunua," Magori alisema.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisisitiza wamemalizana na mchezaji huyo kwa kumpa mkataba wa miaka mitatu na tayari wamelipa kiasi chote cha fedha walichotakiwa na mabingwa hao wa mwaka 1988.

Hata hivyo Ahmed aliongeza Simba imeanza mchakato wa kusaka beki mwingine wa kati ili kuungana na Lawi kikosini hapo.

"Tumeshampata Lawi, kikosini tuna Huseein Kazi , tuna Che Malone na sasa tunataka beki mwingine wa kati ambaye tutamtangaza hivi karibuni kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chetu, tumepania sana msimu ujao," alisema Ahmed.

HABARI UK. 23

9 770856 541002 >